

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,**

**LAMU EAST CONSTITUENCY (KIZINGITI), HELD**

# **AT FAZA SECONDARY SCHOOL**

**ON**

**THURSDAY 2<sup>ND</sup> MAY 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, AT LAMU EAST CONSTITUENCY (KIZINGITI ON THURSDAY 2<sup>ND</sup> MAY 2002**

**Present:**

Com. Ahmed I. Hassan  
Com. Dr. Mosonik Arap Korir

**Secretariat in attendance:**

Programme Officer	-	Tereza Apondi
Asst. Programme Officer	-	Mr. Okeyo
Verbatim Recorder	-	Asha Boru
Sign Language interpreter	-	David Muturi

The meeting started at 9.55 a.m with Com. Mosonik Arap Korir in the Chair. The prayer was said by Sheikh Hashim Mohammad.

**Sheikh Hashim Mohammad :** Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu. Tunakuomba Bwana Mungu, dakika hii utusaidia katika kikao hiki ili tufaulu. Bwana Mungu nakuomba utupe amani na haki na utulivu.

**Com. Mosonik :** Asante sana. Sasa tunaanza kikao rasmi na tukianza, kwanza ningependa kuwajulisha, kwa wanaoleti hapa mbele ambao wametoka kwa tume la kurekebisha Katiba ya Kenya. Na kabla ya hapo ningependa kwanza kuwajulisha mimi mwenyewe, nikianza na Bwana Professor ambayo ni DO wa sehemu hii yenu, Faza Division, wazee wote ambao wako hapa, akina mama, vijana ambao wamesimama kwa madirisha, muingie na kuketi hapa ndani hakuna hoja kusimama nje hivi kuna nafasi ya kutosha.

Ningependa kuanza kwa kuwajulisha kwamba sisi tumetoka kwa Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya. Hapa siku ya leo tuko Makamishna wawili. Kwa mkono wangu wa kulia kuna Kamishna Ahmed Isaak Hassan, ndiye huyu. Kwa tume tuko Makamishna 29, tukiwa hapa leo wale wengine wote wako nasi mkoaa wa Pwani. Wako, Mwatate, Taveta, Matuga, Changamwe, Garsen, Magarini, Bahari na sisi tuko Lamu East. Kwa hivyo msiulize wengine wako wapi? Wako kazini. Tumekuja upande wa Pwani na tutamaliza halafu tuelekee kwingine. Kwa majina mimi ni Kamishna Mosonik Arap Korir, Ama Dr. Mosonik.

Pengine mtataka kujua hawa Makamishna ni wananchi wa Kenya kutoka wapi. Kwa ajili hii ni mara yetu ya kwanza kufika sehemu hii, tumekuja mbali lakini tumefurahi kufika. Kwetu nyumbani ni sehemu za Kericho kwenye chai nyngi. Commissioner useme umetoka wapi halafu niwajulishe wale wengine.

**Com. Ahmed Isaak:** Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu. Kwa majina mimi naitwa Ahmed Isaak Hassan, vile amewaeleza mimi ni mtu, kazi yangu kawaida ni Wakili ni mwana sheria. Nafanya kazi kama mwanasheria huko Nairobi lakini kwa wakati huu nimejiunga na Tume ya Kurekebisha Katiba, kama Commissioner. Natoka mkoaa wa Kazikazini Mashariki. Kwangu nymbani ni Garissa. Lakini leo niko na furaha kuwa na ninyi hapa Faza Island, Lamu. Kweli hapa ni mbali sana, imetuchukua karibu masaa mawili kufika hapa lakini nina furaha kuwa na nyinyi leo.

**Com. Mosonik :** Asante, na ki kazi, mimi ni mwalimu wa Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro ,karibu na Nakuru. Sasa hawa wengine ni wafanya kazi wenzetu, kwanza upande ule mwingine ni Teresa Apondi, yeeye ni Programme Officer anafanya kazi ya Press.

**Teresa Apondi:** Hamjambo.

**Com. Mosonik :** Na anatoka sehemu za Nairobi.

**Teresa Apondi:** Nimetoka Nyanza

**Com. Mosonik :** Nyanza, okay. Na Karibu naye hapa ni Assistant Programme Officer, Mr. Okeyo

**Mr. Okeyo :** Salaam Aleykum.

**Com. Mosonik :** Hata yeye ametoka nafikiri ni Nyanza

**Mr. Okeyo:** Kisumu city.

**Com. Mosonik :** Kisumu City. Upande wa kulia huyu ameketi hapa ni Asha Boru yeye ndiye anarekodi hayo yote mutayasema, inaitwa Verbatim Recorder, awasalimie hata yeye.

**Asha Boru :** Salaam Aleykum.

**Com. Mosonik :** Please the two gentlemen there, can you introduce yourselves first?

**David Muturi :** Habari zenu, mimi naitwa David Muturi – kazi yangu ni sign language interpreter, ya wale watu hawasikii, naongea na wao kwa ishara.

**Co-ordinator :** (inaudible)

**Com. Mosonik:** Asante sana. Yeye ndiye mwenyeji wetu ametuleta hapa na tumefurahi na kazi yake. Sasa kwanza tuelewane hivi: kama kuna mtu ambaye atahitaji usaidizi wa huyu Mr. Muturi wa kutumia ile sign language kwa watu ambao wana shida kusikia, tuone saa hii kama yuko. Yuko mtu wa aina hiyo: Lakini mtu kama huyo akiingia tafadhali mtueleze ndio afanye hio kazi yake. Haya, sasa tukianza tusikilizane kuhusu masharti ya kutoa maoni. Kitu cha kwanza ni kwamba maoni yanaweza kutolewa kwa njia mbili. Ikiwa ni maoni yameandikwa – memorandum, (Written submissions). Yule ana maoni ameyaandika, atapewa dakika tano, siyo lazima aseme, kwa ajili kama ameandika anaweza kupeana straightaway. Lakini kama angependa kusema kidogo, kufafanua, kueleza, anapewa dakika tano. Halafu wale wengine wanasesma, yaani oral submission, ya kusema kwa mdomo bila kuwa na maandiko, tunampa kila mtu dakika kumi.

Lugha tutakazozitumia ni mbili: Kiswahili au Kingereza. Sisi Wabara wengine kuelewa Kiswahili ni ngumu kidogo. Kwa hivyo tunataraji kwamba mkisema Kiswahili, mjaribu kusema Kiswahili kile kinaleweka na Wabara. Lakini kama tutapata shida, tutauliza tusaidiwe na hao wenzetu ambao wako hapa. Lakini kama ungependa kusema kwa Kingereza tafadhali sema kwa Kingereza. Itakuwa mnatuhutubia tume sio wananchi wenzenu, kwa hivyo hata mkisimama, mkinieleza, mnaangalia upande huu. Kitu cha muhimu ni kwamba tuelewe vile mnasema. Mtasimama hapo mbele na mtahutubia upande huu siyo upande ule

mwingine, kwa ajili huu si mkutano hadhara huu ni wa kutoa maoni kwa tume. Halafu, kitu kingine, ni kwamba tunarekodi kila kitu mnasema inanaswa kwa sauti, inaandikwa na verbatim recorder hapa na hata sisi tutakuwa tunaandika hapa.

Haya ukiwa unasema maoni yako mwenyewe, kwanza unaanza kwa kutaja jina lako. Majina nimeyaandika hapa na nitaanza na mtu wa kwanza kujandikisha hapa - - Shariff Hassin. Lakini ukianza, ukitumia microphone, utaje tena ndiojina lako itaingia kwa machine. Na kama maoini ni yako binafsi, useme hivyo, yaani - - Personal views. Kama wewe ni mwakilishi wa kikundi fulani, kama Mohamed Hussein amesema Wayumwali Community, useme ninawaakilisha community, kitu kama hicho.

Halafu mwishowe, ukiwa umemaliza, utaelekea upande ule mwingine na Bi Apondi atakupa register, ujiandikishe kwa register ama ataandika, halafu u-sign ndio tujue kwamba maoni haya ni ya watu wa Lamu Mashariki, sio wengine. Kwa hivyo tunataraji wale wote wako hapa ni watu wa Lamu Mashariki. Ikiwa kuna wengine watakuwa tu observes, wanasililiza. Kwa hivyo nafikiri kila kitu kimeeleweka. Kabla hatujaendelea zaidi, tuulize Bwana DO atusalimie.

**DO of Faza :** Unajua sisi tunapenda kusimama. Tume ya Katiba, nafikiria hawa ni viongozi, wananchi wa tarafa ya Kizingitini na Faza. Nilikuwa naona kama saa hii watu wanakunja nyuso zao sana. Mimi lengo langu la kuwa hapa ni kuhakikisha kuna amani.

Kitu cha pili nikuangalia mwongozo wenyewe umewekwa unafwatwa na hakuna mtu mwenye atakatazwa kutoa yale maoni yeye yuko nayo. Lakini kuna watu wenyewe tutakuwa nao, kuna ile kulalamika na kutoa maoni, tuangalie tofauti. Kuna kitu ingine, kwa sababu pengine saa zinaweza kuwa chache, tuangalie tukitaka twende haraka na kila mtu asikizwe, ni kuangalia mahali penye mtu atakuwa anaongeza, tukikuwa na kurudia tutachukua wakati mwingi.

Commissioners karibu Faza. Watu wa Faza Kizingitini na vijiji vyake ni watu wenyewe amani. Hata pengine hizo vijiji vikiwa mbali, nafikiria kuna mtu mwenye anatoka kwa vile vijiji na nafikiria maoni yatakayo tolewa ni ya watu wa Faza na Kizingitini. Nilikuwa nataka makae mjisikie huru wenyewe watatoa hiyo maoni watoe yote sawa sawa. Kwa sababu walisema nyinyi ndio Swahili, mnasema maji yakimwagika, hayazoleki tena. Asanteni.

**Com. Mosonik :** Asante, kwa hivyo tuanze na Shariff Hassin

**Shariff Hassin :** Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu – Mimi natoa maoni yangu binafsi, maoni ya kwanza.

**Com. Mosonik :** Na useme jina tena.

**Shariff Hassin Mohamed:** Shariff Hassin Mohamed.

**Com. Mosonik :** Endelea, endelea

**Shariff Hassin Mohamed:** Chief Kadhi, ningeomba kwa maoni yangu ya kuwa awe na naibu. Maana yake Chief Kadhai wakati huu hana naibu. Akiwa hapo nafasi yake inachukuliwa na Kadhi ya Wilaya ya Mombasa. Kwa hivyo twataka naibu wa Chief Kadhi kwa Kenya mzima.

**Com. Mosonik:** Endelea

**Shariff Hassin Mohamed:** Pia Chief Kadhi ateuliwe, sio kupewa na serikali, ateuliwe na Ma-Imam. Chief Kadhi na Machief Kadhi wateuliwe na Ma-Imam wa Misikiti, sio kuchaguliwa na serikali na kupewa.

**Com. Mosonik:** Endelea—

**Shariff Hassim Mohamed:** Na apewe hukumu yeye mwenyewe sio kupeleka high court. Mambo ya kiislam yasipelekwe high court, yeye amalize.

Uhuru wa dini tulio nao isibadilishwe, maana yake tuna uhuru wa kuabudu, serikali imetupa, isibadilishwe kabisa, kwamba bila uhuru wa kuabudu inaweza leta taabu sana. Vipindi vyta dini ya Kislamu katika radio ni kidogo sana. Twaona dini zingine wana nydingi sana, na kama dini zingene nasi tupewa nafasi sawa sawa katika vipindi hivi vyta dini ya Kislamu katika radio.

Uvuvi ni muhimu sana kwetu, tunaiomba serikali isiweke vikwazo kwa kuvua. Isaidie serikali ipatikane soko la kuwekea samaki watu wapate mahali pa kuuzia. Serikali tunaiomba iwape makao bora, wavuvi. Maana yake hakuna kazi nyingine huku Pwani, katika division hizi mbili au tatu.

Elimu iwe bure kwa watoto, hawa kwa watoto mayatima wasaidiwe maana yake wazazi wao wamefariki.

Mwisho, akina mama wapewe haki sawa na waume kwa kazi na elimu.

**Com. Mosonik:** Asante, nakushukuru, upitiye hapo tafadhali na usign vile nilieleza muwe mukipitia hapo. Mwingine ni Najim Shaffi.

**Najim Shaffi :** Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu – Haya ni maoni yangu binafsi. Jina langu ni Najim Shaffi kutoka Tchumba location. Maoni yangu binafsi nikuelezea kuhusu Chief Kadhi.

Ya kwanza, kuhusu kuchaguliwa Chieh Kadhi na naibu wake, ningependelea wachaguliwe na wasomi, wasichaguliwe na

serikali. Kwa maana ndio unaona kila mara tunapopata kwamba, kuhusu Chief Kadhi, kuwa alifanya kuwekewa na serikali jambo kama hili ni mistake.

Halafu na jambo lingine, tunaomba Chief Kadhi apewe uhuru kamili wa kuhukumu. Awe na sheria kama judge, kwamba mambo mengi ya Kisalamu ayahukumu moja kwa moja bila kupitia kotini, ambapo akiwa judge, Kadhi awe wa kumaliza mambo yetu ya kiislamu.

Halafu, jambo la pili, ni kuhusu kuchakuliwa viongozi: tungeomba serikali yetu kwamba mtu ambaye si mukenya halisi, ambaye si mzaliwa wa nchi hii ya Kenya awe hatachaguliwa kuongoza nchi yetu awe ni mzaliwa wa Kenya halisi siyo awe mtu wa makaratasi.

Jambo la tatu, sisi huku kwetu ni wakulima. Tungeomba serikali itusaidie kama wenzetu wa bara vile kama majani chai wanaauza nchi za nje, sisi hapa kwetu tuna vitu kama makoma, ufuta, korosho, tungeomba serikali watupatie soko kama wenzetu.

**Com. Mosonik :** Asante, mwingine ni Shariff Sabik Ahmed

**Shariff Sabik Ahmed :** Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu, jina langu kamili ni Shariff Sabik Ahmed kutoka Chintu – Chairman wa KANU.

Maoni yangu mimi nataka kutoa upande wa mali ya asili: Mali ya asili imeletwa na mwenyezi Mungu, haikuletwa na binadamu kwa dunia nzima, ingawa sisi tutazungumzia Kenya. Mwenyezi Mungu ameleta mali yale kwa wananchi kwa manufaa yao. Kwa hivyo inatakikana mali ya asili iwe mikononi mwa wananchi, uwezo uwe kwa mwananchi, uchungaji uwerekwe katika wizara yenye kuhusika. Kwa sababu mali ya asili iko na sehemu nyingi: kuna bahari, Ardhi, mkopo, madini kufukuliwa. Kwa hivyo wizara kama ya ukulima: ukulima una sehemu mbili kuna ardhi mbaya, kuna ardhi yenye kutoa mazao. Ikiwa uwezo hautawekwa kwa wananchi, wananchi hawataweza kujichagulia mahali ambapo kumekufaa ukulima bora, kama nchi inapofanywa sasa. Tukitaka kuweka park, sisi wenyewe ndio tuseme park iwekwe hapa, ukulima uwerekwe hapa. Tukitaka kuvua katika bahari, tuseme bahari ivuliwe iwavuvi wakuwe hapa au park ya wavuvi iwekwe mahali pale bila kuwekwa kwa watu wengine. Tukiwa na mikopo pia wananchi wanaweza kutumia vile ambavyo itawathibika isiwe na uwezo kwamba huwezi kutumia mikopo mpaka uombe hurusa kwa mtu fulani. Wananchi wenyewe wakitaka kutumia mikopo wawe na uwezo wa kuitumia.

Kama wanyama – Wanyama wamepasishwa na Mwenyezi Mungu waliwe. Lakini tunaona sisi tumestahilishiwa wanyama fulani: mbuzi, ng`ombe, kondoo, lakini chope hatuwezi kula, nyasi hatuna ruhusa kula, kapa hatuna ruhusa kula, kivuva hatuna ruhusa kula. Kwa hivyo ni wajibu wetu sisi kulingamana na ubinadamu tupatiwe nafasi hawa wanyama wote vile tunaweza kuwatimia -. Ikiwa uwezo wa mali ya asili utawekwa mkono wa wananchi.

**Com. Mosonik :** Asante sana. Khadija Shariff kwa niaba ya kikundi aakilishe

**Khadija Shariff :** Commissioners, wageni, mabwana na mabibi, Salaam Aleykum. Naanza kwa utangulizi: ningependa kuwa kwenye katiba ianze utangulizi yenyе kumfahamisha mwananchi namna.

**Com. Mosonik :** Sasa, please sijui pana shida gani, jina lako, tena utueleze umeandika, unasema kwa niaba ya group, which group is that?

**Khadija Shariff :** Mimi naitwa Khadija Shariff, niko hapa kwa niaba ya Swathinia Women group, Kizingitini.

Maoni yangu ningependa Katiba ianze na utangulizi ambao utamfahamisha mwananchi na iwe ni lugha, si ngumu sana kueleweka. Pia sisi Waislamu mwongozo wetu au katiba yetu, tunaongozwa na Quran, ningependa hivyo hivyo mambo ya ndoa, talaka, urithi, tuendelee kuhukumiwa vile kwa Quran.

Upande wa Bunge – Tungependa kuwa Wabunge wawe watahusika kugakua maafisa wa serikali na pia wa mashirika. Kazi ya wabunge iwe ni vile vile saa maalum, lakini iwe mbunge atatembelea eneo lake mara tatu kwa mwaka. Wananchi wawe na uhuru na haki ya kumregesha mbunge au diwani kwa kura ya maoni. Na Katiba pia ioneshe tarehe za kufunga bunge, tarehe za kura - - ionyeshe kura zitakuwa lini na bunge litafungwa lini. Na pia tungeomba kwenye bunge waongeze nafasi kwa upande wa wanawake, wapate kuakilisha wanawake wenzao. Walemvu wapate wao kutoa shida zao kama upande wa elimu na upande wa kazi. Vijana wao wapewe nafasi ya kueleza matatizo yao. Watu wa dini wawe na kiongozi kwenye bunge. Pia marginalized group, minority - - wale watu ambao ni kidogo, wapate kuweko kwenye bunge kuakilishwa.

Upande wa mahakama tungependa maafisa wa mahakama wakae mahali kesha miaka mitatu kabla kuhamishwa, kupewa transfer.

Upande wa Kadhi: Kadhi achaguliwe na viongozi wa dini na Kadhi Mkuu achaguliwe na Kadhi. Pia tungependekeza kuwe na Senior Kadhi na assistant Kadhi, na Kadhi apewe power zaidi kuliko kwenye Katiba ya sasa, awe ataingilia sio mambo ya ndoa na talaka na urithi, awe pia ataangalia social problems, mambo ya kuiba na mambo ya watoto, badala ya watu kwenda ofisini ya watoto. Kadhi pia aruhusiwe kukata rufani.

Upande wa Ardhi: tungependelea kuwa ardhi ziwe communal land sio Government land. Wanaume na wanawake wawe na haki sawa kumiliki ardhi. Na ugawanyaji wa ardhi lazima upitie kwa wazee wa mji. Na tena wale kwenye committee wawe ni watu wa pale pale sio watu wa nje. Kabla Title Deed haijatoka lazima hawa watu wajulishwe. Na ikiwa ni ardhi ya mtu binafsi lazima serikali inunue ardhi ile kwa mtu isichukue bure. Ugawanaji wa ardhi utategemea baina ya watu na ukubwa wa ardhi,

hatuwezi kusema itagawanywa kivipi.

Haki za kimsingi tungependelea kuwa haki za mzingi zinazo faa kwenye Katiba iwe ni upande wa usalama, hudumma za afya, maji, elimu, makazi, chakula na ujira.

Upande wa elimu: tungependelea kuwa elimu watoto wapate msingi bora na wasomeshwe elimu iwe ni bora, mpaka ikiwezekana primary school. Ikiwa mtoto ameonekana hi hodari serikali pia imsaidia katika shule ya upili. Walimu wa madrasa pia tungependekeza wao walipwe mishahara kama walimu wa skuli na serikali. Pia tungependekeza kuwa wanafunzi ambao wanaenda national school wasilazimishwe kusomeshwa Christianity, pia wapewe uhuru wa kuvaan nguo zao kama hijab. Kuna skuli zingine mpaka sasa hawajakubaliana na mambo ya kuvaan hijab. Pia ningependekeza kuwa civic education iendelee kusomeshwa kwa public na maskuli iwe ni katika lesson ambapo watoto wetu wakiinukia watajua wanasomeshwa nini na itakuwa ni rahisi kuifwata. Mashule pia kuwe na vifaa vinavyofaa kwa sababu watoto wetu si wajinga vile kuna ukosefu wa vifaa.

Tungependelea wa upande wa kuaajiri kazi lazima 75% ya ile kazi wapate watoto wetu kuliko kuletewa watu kutoka nje.

Upande wa walemaru lazima wapewe elimu ya bure na kazi pia wapate kujisaidia wao wenyewe.

Upande wa headmen pia wana haki na wao kwa vile wana saidia serikali walipwe mshahara kidogo kwa sababu wengine hawana kazi, wanategemea kazi hiyo hiyo.

Upande wa marginalized group wapewe waakilishi wao wapate kutoa malalamiko yao.

Na watoto wetu ambao pengine wamepata bahati wameingia upande wa madawa ya kulevia, lazima wasipelekwe jela kubwa, wapelekwe rehabilitation centre, serikali waangalie centers wapate hawa watoto kusomeshwa kuliko kwenda kutoa adhabu kali.

Pia ningependekeza kwa upande wa elimu kuwe na college kila district na university kila wilaya.

Wanawake waliofiliwa wapewe eda period na mshahara kwa juu, kwa sababu hii ni upande wa dini si kupenda kwake, mtu akimaliza eda ambiwe kazi huna. Kwa hivyo tungependelea tupewe eda leave na pia tulipwe mshahara. Wanawake ambao wameachwa na mabwana zao kwa kifo ama pengine wameachwa juu bwana ameo a bibi mwagine, lazima wale watoto waangaliwe ki sawa sawa kwa upande wa elimu na mavazi.

Katiba lazima iliinde haki ya watoto: wasipewe kazi ngumu na kulazimishwa pengine kufanya kazi ambazo wao hawangependelea.

Upande wa mali ya asili na rasilimali: ningependelea kuwe kuna sheria ya watu wasiruhusiwe kusafirisha vitu vya mali ya asili kama antiques zipelekwe nje. Pia kuwe na sheria vile vitu ambavyo viko nje viregeshwe Kenya kwa sababu pengine wamevichukua kwa dhuluma na pengine vitu vile hazipatikani tena Kenya.

Upande wa mikoko: kuna miji mingine hapa ambao watu wanategemea mikoko ndio rasimali yao. Pia tungependelea mikoko iwe preserved. Hatutaki kuwa, tuseme ikatwe yote lakini pengine wangeshauriwa watu ikatwe upande moja na upande moja mikoko iendelee, kwa sababu wale watu ndio uchumi wao kupata maisha.

Upande wa uvuvi: ningependelea serikali kuwa wawape ujuzi zaidi wavuvi wapate ujuzi wa kuvua samaki zaidi. Pia wasiweke vikwazo vingi kama hizo nets, pengine, nets number kumi ama ngapi. Serikali isitoe license ama ruhusa kwa meli hizi za China trollers zije zivue samaki ambao watu wa hapa hapa watapata taabu.

Upande wa wakulima, hapa tuna makao mengi kama simsim, makopa, na kwa bahati mbaya hatuna soko. Kwa hivyo tungependelea pia bidhaa zetu ziuzwe tupate soko na tupate faida zaidi.

Pia hizi rasilimali zetu ambazo zinatoka kwetu, tunataka 80% zifaidishe watu wa pale pale kuliko ifaidishe serikali. Bunge liwe litasimamia hukusanyaji wa pesa hii, na hiyo African cake ikija zote na sisi tupate sawa sawa kama wale watu wengine.

Kuwe na tume ya huduma kuondoa ufisadi iangalie kama ufisadi umemalizika ama bado.

Uchaguzi: Kuwe na utaratibu wa uchaguzi mzuri. Ikiwa kura ni tano wanawake wapewe angalai kura tatu na wanaume kura mbili, wasiwekwe nyuma wanawake. Kusiwe na idadi ya watu kama percentage fulani kuambiwa kuwa mtu ndio atachaguliwa awe Mbunge na rais, hiyo iondoshwe.

Kwa madiwani pia, tusiwe na percentage fulani, kwa sababu minority, wale watu wadogo wanapata taabu na wameonewa. Pia sio lazima madiwani wawe na elimu kubwa sana, muhimu ni kuwa wakilishi wazuri, si lazima wawe wamesoma sana, bora wawe wanajua kusoma na kuandika.

Kuwe na waakilisha zaidi, mfano kama hapa Lamu, tunao Lamu East na Lamu West. Tungependelea pia ikiwa tutakuwa na Lamu Central ipate kuakilishwa zaidi na kuwfafikishia watu zaidi.

Pia tungependelea kuwa tarehe ya uchaguzi itiwe kwenye Katiba na Rais achaguliwe moja kwa moja na wananchi na akisha kuapishwa wakati ule ule rais aanze kazi yake. Rais awe na miaka arobaini na awe na degree. Majukumu ya rais yatiwe kwenye katiba watu wajue kazi yake ni nini.

Mayor wa mji achaguliwe na watu, na clerk to the Council ndio achaguliwe na madiwani.

Utawala wa mikoa, uwe utachaguliwa na wananchi, ku-present wale watu wenyewe wanataka.. Asante.

**Com. Mosonik :** Tusipitishe dakika kumi ama tano ukiwa una memorandum. Sasa ningependa Zuena Mohamed Asin, Zuena Mohamed, hayuko? Yuko?

**From the floor :** The other one has already spoken on her behalf.

**Com. Mosonik :** Asante, sasa tutamsikiliza Mohamed Ali kwa niaba ya Kizingiti na yeye ameandika. Utatupea memorandum ukimaliza, please.

**Mohamed Ali:** Jina langu ni Mohamed Ali kutoka Divison ya Jumbo – Tunataka serikali ya majimbo.

Ardhi ya Dodori serikali iachie wenyewe mabajuni, serikali iwe ni muhifadhi. Tunataka eneo la Faza Island, toa mbili, moja, na baadaye kila mtu achukue ardhi yake. Iliyobaki iwe ni Mabajuni wenyewe watakakubaliwa.

Tatu haki za kienyeji za ardhi zikubaliwe kama zote mbili. Ardhi za serikali - zisigawanywe kiholela bila wazee wa mji na taifa kujua. Mwenyeji wa mji awe na nafasi ya kwanza kupewa ardhi kama hiyo.

Bahari – hawking ya aina ye yeyote iondolewa baharini naardhini. Wavuvi wasidaiwe kwa mikopo na bombo za kisasa za kuvulia. Wavuvi wawekewe usalama, ulinzi (security). Faida ipatikanayo katika samaki wapewe wavuvi. Mkopo na watiwe raia ile wadhuruku vile wanavyotaka. Faida ya mikopo wapatiwe raia. Kiwa mwananchi halisi aruhusiwe kuvua samali bila malipo ye yeyote. Aina ya samaki ye yeyote apatikanao baharini, liwe si kosa hata awe ngumo. Wakulima: Mazao yapatiwe soko kama vile majani na kahawa.

Katiba – Katiba iandikwe kwa Kiswahili na Kingereza, Katiba iwe ni somo mashulen kama vite hesabu na Kingereza ili watoto wajue Katiba ya nchi yao.

Wahalifu – Wahalifu wakishikwa wasiwekwe cell kama muda wa masaa ishirini na nne. Wahalifu wakishikwa, wasipigwe na polisi, wasilalishwe na pingu.

Umilikaji wa vitu - Waislamu wasisumbuliwe katika umilikishaji wa vitu kama passport, birth certificate, na vitambulisho.

Bunge – mbunge ye yeyote asiyefika katika eneo lake la bunge kwa muda wa miezi mitatu ajue wazi kuwa kiti chake kitakuwa

wazi. Mbunge yeote asiyefanya maendeleo katika eneo la bunge kama muda wa miaka miwili ajue wazi kuwa kiti chake kitakuwa wazi

Wabunge – wenyе kusimamia ubunge wawe ni wazalendo si wageni, wawe wenyе tabia nzuri ambaо wanajali masilaha ya wananchi.

Machief – machief wasichaguliwe wakiwa wadogo.

Maji na umeme, serikali ituletee maji na umeme katika eneo la Lamu District.

Uchimbaji wa madimu – uchimbaji wa madimu waachiwe wananchi.

Elimu – elimu iwe ya bure.

Matibabu ya bure.

Kadhi court – Kadhi awe amesoma sheria, Islamic law, achaguliwe na kamati ya wanavyuoni, apewe mamlaka zaidi kama majaji wengine, yaani magistrate.

Kura – kura iwe ya siri na madebe yawe ya kuonyesha (transparent). Kura ihesabiwe kituoni. Kabilia la Kibajuni litambuliwe serikalini kama kabilia.

**Com. Mosonik :** Asante. Ahmed Lali. Tueleza group ni gani, please.

**Aхmed Lali Ahmed :** Salaam Aleykum wa Rahmatuhillahi Wabarakatu, mimi ni Ahmed Lali Ahmed nikitoka Kizingitini. Maoni yangu yapitia kwa Mwafaka Group. Maoni yetu ya kwanza ni: Katiba liwe ni somo mashulenі na iwe ya Kiswahili.

Pili, taifa la Kibajuni ni mojawapo katika mataifa 42, lakini masikitiko ni kwamba halipatiwi haki za msingi kama makabila mengine yanavyopatiwa. Kwa mfano kama umilikaji wa ardhi: taifa la Kibajuni halina mpaka leo. Katika haki za kimsingi ambaо halipatiwi: Ukilima - Wabajuni walima ukulima wakijadi, serikali haiwashugulikii kuwapatia ukulima wa kileo.

Uvuvi – Mbajuni kutoka azaliwe mpaka leo amekuwa kwa uvuvi ule ule wa majadi, serikali haimshugulikii kumpatia uvuvi wa kileo. Matibabu - Wabajuni mpaka leo hivi hawapatiwi madaktari wakutosha wenyе kuwashugulikiwa afya zao, wala haiwapatii madawa ya kutosha, madawa muhimu yenye kuwasaidia afya zao. Sisi tuko mbali na Lamu au tuko mbali na sehemu zingine. Bajuni safari mumeiona kutoka hapa visiwani, ziwa la Faza mpaka kufika Lamu, umbali wake. Mbajuni asafiri kutoka hapa

visiwani Faza mpaka kufika Lamu pengine kupima damu. Kwa hivyo Katiba hii mpya tungependa Mbajuni apatiwe haki zake.

Barabara – Barabara ni kitu muhimu katika taifa la Kibajuni, barabara hii ya lamu. Barabara ilizorota kutoka siku ya mvua nyingi iliponyesha na pesa tukasikia zimetolewa, barabara mpaka leo mbovu. Kitu ya kusikitisha, hivi mvua ikinyesha, sisi tunaumia biashara zinapata hututi zaidi ya mara mia.

Mambo ya kidini – Tungeomba katika Katiba mpya mambo ya kidini yaheshmike zaidi na zaidi, yakiguzwa mambo ya kidini ndio ameguzwa muislamu. Hapo ndipo muislamu ataamuka., kisha lawama isiwekwe kwetu.

Hongo – Tungependa Katiba mpya itunge mambo ya hongo na ufisadi. Katika nchi yetu ya Kenya hongo na ufisadi vimezidi, vimezidi na mpaka ndio nchi yetu ikaletwa katika hali hii ya kuzorota kimaisha au kiuchumi.

Machief Kadhi: Machief Kadhi ningeomba, katiba iwaangalie au iwachague kwa kupitia kwa watu wenye elimu ya kutosha ndiyo ichague Machief Kadhi, isiwe serikali wanaingilia kitu ambacho hawakijui.

Elimu: elimu katika nchi yote ningeomba iwe ya bure.

Sheria ya nchi; ikiwa imewekwa sheria ya nchi yoyote, sheria ile imuguze kila Mkenya isiwe itamguza maskini, mtajiri imuache. Isiwe itamguza raia, mtawala wa machief kama DO, DC, PC imuache. Mimi nikimtukana DC isiwe kwamba mimi nativa pingu. Mimi nikimtukana DO nawekewa pingu, lakini DO akinitukana mimi hajui pingu. Kwa hivyo sheria imuone kila mtu.

Mapigo: mapigo polisi tungependa yakome. Si kila mtu huwa anapenda kushikwa, afikishwe polisi, apelekwe mahakamani. Mahakama impate na makosa imfunge au imkose na makosa imuwashilie, lakini kumpiga kumuumiza hii si katika haki za uraia.

Mambo ya ardhi – mambo ya ardhi, kwanza kama nilivyosema sisi wa Bajuni tumekosa haki ya kumiliki ardhi serikali ijapo itkubalie kutupa haki za kumiliki ardhi. Kwanza mambo ya ardhi iangaliwe mkaazi wa ile sehemu. Sisi masikitiko sehemu zetu hizi nyingi zimechuguliwa na watu si wakaazi wa hapa.

Haki ya bahari – haki ya bahari imetuumiza sana. Leo tumekua tukija baharini twavua twambiwa hapa msivue. Hapa kunabaki, hapa msivue imetuumiza. Kwa maana sasa pahala kuna mazao zaidi tumekuwa hatuwezi kuvua, tukienda kuvua pahala ambapo hakuna mazao, ndio njaa kwetu imezidi.

Bara – haki ya bara hiyo ndio imetuangamiza kabisa. Wametuwekea nafasi ndogo ya ukulima nafasi ambazo hazina rutuba, zile ziko na rutuba, zimekaa hazina faida kwa serikali hazina faida kwetu. Ni wanyama na wakora, majangili wakija kujificha hapo wakitufanya sisi wakulima ugaidi. Kwa hivyo tungependa hii haki ya bara iondolewe mbali, nafasi ya bahari kathalika iondolewe

mbali.

Kiongozi – Kiongozi yeote wa nchi ikiwa ni rais, mbunge, diwani, akisha amekuwa ni raia kwa njia zozote zile, achaguliwe kwa sifa. Ikiwa anazo sifa za kuchaguliwa, achagiliwe, aweza kuwa ni mzaliwa lakini sifa za kuchaguliwa hana. Kwa hivyo sifa za mtu awe kiongozi mwenye imani na watu wake, awe mwenye hurumma na watu wake. Kwa hivyo kiongozi wowote achaguliwe kwa sifa zake, anastahili kuchaguliwa au hatasitahili kuchaguliwa?

L:a mwisho serikali iwe ya majimbo. Kila sehemu iwe na jimbo lake, na sisi Wabajuni ndio tutaweza kufaidi.

**Com. Mosonik :** Hamid Mohamed.

**Hamid Mohamed:** Salaam Aleykum. Kwa jina ni Hamid Mohamed. Kwa maoni: Kwanza tulikuwa tulisema serikali iundwe ya mseto.

Ya pili, tumesema watawala wa mikoa wachaguliwe na wananchi.

Rais awe na majukumu haya: jukumu la kulinda usalama wa nchi, jukumu la kuongoza sherehe za kitaifa, jukumu la kuwachagua mawaziri na wanaibu wake, na jukumu la kulinda masilahi ya wafanya kazi.

Hivyo lazima pia maafisa wa mahakama wachaguliwe na kamati ya bunge. Ma-Judge nchini Kenya wachaguliwe na wanachuoni.

Nasema meya na mwenyekiti wa county council wachaguliwe na raiai. Mishahara na marupurupu ya madiwani ishugulikiwe na kamati ya serikali ya wilaya. Kisha si lazima madiwani wateule waondolewe katika katiba hii.

Hukumu ya kifo iondolewe.

Tuwe na lugha mbili ya Kiswahili na ya Kingereza ibaki hivyo hivyo.

Pia tunapendelea mfumo wa serikali ya majimbo.

Katibu mkuu wa kila wizara awe na mamlaka ya serikali kabla ya uchaguzi.

Wabunge wafanye kazi siku zote za wiki, watengewe siku maluum za kwenda kuwatembelea watu wao. Mbunge asipotimiza ahadi hiyo ajue kwamba sheria ya kisawa sawa imechukuliwa.

Polisi wapatiwe mafunzo zaidi jinsi ya kuwahudumia wahalifu.

Mali ya asili iwe mikononi mwa watu wa eneo lile.

Pia tunasema sheria itumiwe kwa wananchi wote wa Kenya hasa maafisa wa serikali.

Mpangilio wa elimu usiwe wakubadilika mara kwa mara na ikiwa ita fanyika kwa dharura basi tuwe tuna kamati ya kubadilisha mambo hayo.

Pia tunasema elimu, huduma za matibabu ziwe bure na sawa kila mahali.

Makabila yote Kenya yachukuliwe sawa bila ubaguzi wa aina yeyote.

Mbunge yeyote ambaye atatoa ahadi katika jukwa la siasi, kisha asitimize ahadi ile, basi ashtakiwe.

Kisha tunasema mgeni yeyote asinunue ardhi ya watu bila dhamira yake kujulikana.

Walemvu wasibaguliwe wapewe haki kama watu wengine.

Watoto wanaorandaranda mitaani wahrurumiwe na serikali.

Waallimu, watu wa usalama na matabibu walipwe mishahara bora kuliko wafanyi kazi wengine.

Wahalifu wasicheleweshwe kuhukumiwa.

Baraza la mawaziri lipunguzwe hadi kumi.

Kuna tume nyingi sana katika nchi kwa hivyo zipunguzwe.

Idadi ya wabunge pia ipunguzwe hadi 188.

Sheria ya eda ipitishwe kwa wanawake wa Kislamu walioandikwa kazi na serikali.

Tuwe na tume ya kusimamia ujisadi.

Rais apunguze wajumbe wake wanapokwenda safari za ng' ambo. Rais awe amechaguliwa na watu wengi.

**Com. Mosonik :** Nikuulize, tena ulikuwa unasema kwa niaba ya kikundi kipi?

**Hamid Mohamed:** Na kwa niaba ya community ya (inaudible)

**Com. Mosonik :** Na ulikuwa na memorandum? Tafadhali upeane. Nyabane Sheik Ali Mohamed, yuko?

**Nyaban Sheik Ali Mohamed :** Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu,

Mimi haja yangu inaonileta katika hii Katiba. Naomba wanawake nasi tusiwekwe nyuma,tusidharahuliwe. Hakika hapa kwetu sisi, ikitokea kazi iandikwe vijana tupu. Nataka mimi niandikwe kazi. Kazi yeoyote ikija tufanye waswahili, tufanye vijana wa kwetu.

Mazao yetu ni ukulima, mkulima lakini hana bei. Hata tukalima sisi vijana wetu waweze kupata kitu, hazina masoko vitu vyetu(inaudible). Lakini naomba kwa vikundi vyetu sisi wanawake tusaidiwe kwa mikipo, mtusaidie kwa uwezo wenu mlionao tuweze kunawiri. Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu.

**Com. Mosonik :** Mohamed Hussein – wa Wajimwali community.

**Mohamed Hussein:** Mimi nitatumia lugha ya Kingereza.

**Com. Mosonik :** Tafadhali tuelewane, maoni. Excuse me, listen, maoni yanatolewa kwa tume na yeye anahaki kusema kwa Kingereza. Tafadhali, please.

**Mohamed Hussein:** My name is Mohamed Hussein presenting constitutional views from Wajimwali sublocation: Okay.

Preamble – The people of from Wajimwali say they would like to have a Constitution that would generate unity, peace, love, justice and prosperity. They also need a constitution which will capture the national philosophy and guiding principles.

They said the new Constitution should retain the view which allows the Parliament to amend any part of the Constitution by 55% majority vote, but the public should be involved through referendum in amending the Constitution.

On citizenship: According to the people of Wajimwali they said the new Constitution should not allow anybody to become a citizen of two nations simultaneously.

The government should ensure the provision of Passports and ID cards to all her citizens without any restriction and without any such stress.

Third, a foreigner who has been married by a Kenyan citizen, and lived in Kenya for a period of 5 years should be given citizenship without restriction or discrimination.

Fifth a child whose one of the parents is a Kenyan should be regarded as a Kenyan citizen.

Defence and National Security – On this issue Wajimwali people said that: defence and national security should be in the hands of the Parliament and not the Executive including the president. The Government should provide security to all her citizens in any part of the country, and ensure that people live in peace, without fear. Third, homeguards should be deployed in areas where security personnel is inadequate.

Political parties: They should play roles like political mobilization in National building and in executive composition. The Constitution should not allow any defection of a member of a party more than three times consecutively. The Constitution should allow the registration of only 3 political parties. MPs from either political parties should be included in the cabinet composition that is coalition government.

The Legislature - There should be a moral and ethical qualification for a Parliamentary candidate. Second, there should be a special salary review commission for MPs and other Parliamentary workers. Third, there should be no nominated MPS. Fourth, the people reserve the right to recall their MP through by-election. MPs should be in full time occupation, that is, from Monday to Friday, like any other government worker. The Constitution should permit coalition government. The Constitution should not allow the President to vet the legislation passed by the Parliament. The Constitution should not permit the President to dissolve the Parliament till the end of its tenure.

The Executive – The new Constitution should not allow the president to be above the law. The power of the President should be limited, e.g: like in the appointment of the Attorney General, Permanent Secretaries, Chief Justice and Executives of the Electoral Commission, instead the Parliament should assume the power. The new Constitution should provide for the removal of the President through the vote of no confidence when he or she is in office, when he is involved: in shady deals, in corruption, mass killing, or chronical health - - problem physically and mentally. The new Constitution should not allow the President to conduct foreign affairs, including making treaties, without the consent of the Parliament. The new Constitution should not allow the President to - - - the preservation of public security act, under which serious restriction can be placed on rights of freedom of Kenyans, including detention without trial. The new Constitituion should allow the President to be taken to court in criminal or civil matters, while in office.

Judiciary – The Constitution should allow a supreme court. There should be a Constitutional court. The judicial officers should be appointed by qualification. The tenure of judicial officers, should be 5 years only, subject to reappointment regarding one's conduct.

Kadhis should be elected by delegates of muslim scholars. Kadhis should play similar roles as the magistrates and judges. Kadhis should be well learned and conversant with both circular laws and religious laws. There should be provision for Judicial review by the Legislature.

The Local Government – Mayors and Chairmen should be elected by people. Mayors and Chairmen should possess “O” level education, at least.

**Com. Ahmed I. Hassan :** Let me interrupt you, I just want to say that since you have a written memorandum, just highlight the issue. When you are highlighting please, you will tell us again about the three political parties. You are saying that there should be only three political parties, we would like you to tell us which three.

**Mohamed Hussein :** Which parties? I cannot name which party. This will depend on the majority. We don't want so many parties in Kenya because this creates things like tribalism - -where every tribe is forming its own. It is because of that that we want only three political parties. I am reading because there might be problems, may be you will be numbering, then they give you problems.

**Com. Ahmed Hassan :** No, no, it will not, just highlight.

**Mohamed Hussein :** There are so many things to be discussed because I am going topic after topic, therefore I am submitting this memorandum on behalf of the community of Wajimwali people. Thank you.

**Com. Ahmed Hassan :** I would like you to stay, just before you go so that wananchi wasikie. You have said local government, what else do you have on local government?

**Mohamed Hussein:** The remaining topics are on local government, basic rights, individual rights, land and property, management and use of natural resources - - and this is a very sensitive issue, this area, Environment and Natural resources, and the structure of the government. Also there is participatory of governance, separation and transfer of power, and the last topic is on the Structure of the Government.

**Com. Ahmed Hassan:** I am not going to continue with the dialogue but the one that you are saying is sensitive can you just highlight very quickly.

**Mohamed Hussein:** Okay there are two main topics here: One- Management and use of Natural Resources. In our new Constitution, there should be fair distribution of natural resources among the Kenyans. That is in managing, control, and use of natural resources. This should be under the control of the people, not few individuals or the government. They also said, on the same issue, foreigners should not be permitted to exploit the natural resources for their own benefit. The example we have is the Japanese coming here and destroying our fish.

They said public officers should be required to declare their assets before they hold any public office. Then, there should be a code of ethics for the holders of public office.

Environment and Natural resources, it is very important: The new Constitution should ensure the provision of civic education on environmental protection issues. The local people should be fully involved in setting by-laws on the protection of their environment. The council of elders should have the powers to enforce laws on protection of the environment. The natural resources should be owned by the local people of a given geographical area. The role of the community in the Constitution shall be to: conserve, protect, and manage the natural resources, but not the government or any other organization. Thank you very much.

**Com. Ahmed Hassan:** Lali Kasimu Bunu.

**Lali Kasimu Bunu:** Salaam Aleykum wa Rahamtuilahi Wabarakatu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu. Jina langu ni Lali Kasimu Bunu, nikitoka Kizingitini location. Area Councillor - - Kizingitini ward.

Maoni yangu: Kwanza Sheria ya Kisamu isiingiliwe na serikali. Kwa sababu Uislamu ni mwongozo uliotoka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu ukipitia kwa Mtume Mohamed. Kama vile mambo ya ndoa, talaka, wirathi, kwa hali hiyo yasiingiliwe kabisa. Vile vile kuna ma-Kadhi, kuna na manaibu wa ma-Kadhi, makadhi wanalipwa na manaibu wa kadhi hawalipwi. Kwa hivyo Katiba hii mpya, inataka ipitishe manaibu wa Makadhi walipwe kama vile wanavyolipwa Kadhi.

Vile vile tunataka serikali ya majimbo, ili mapato yanayopatikana katika bandari kuu yetu ya mkoa, yabaki na sisi tu huku. Hivi sasa tunasikia tu kwa Katiba hii tulio nayo kuwa ati bandari inatoa mapato na sisi hatuyafikii. Kwa hivyo Katiba hii mpya, tunataka tupatiwe serikali ya majimbo ili mapato yale ya mkoa wetu yatufaidishe sisi wenyewe. Nafasi za kazi kama zile za Navy, kwa Katiba hii mpya, watoto wa Coast ndio wajuzi zaidi kutembea baharini kuliko mwengine yejote katika nchi hii. Na hivi sasa tunataka Katiba mpya ikiwa yenyе ukweli, maana tumeona Kamishen nyingi zinakuja na yale tunazungumza tunajua yako hapo. Kwa hivyo tunataka nafasi hizo za Kenya Navy wapatiwe watoto wetu kwa sababu ndio haba kule baharini. Kama watoto wa Kizingitini wanaenda kuzamia futi ishirini na nne, futi mpaka hamsini, halafu kazi hizo wawe hawatapatiwa, ni thuluma kubwa kwa Katiba hii tulio nao. Kwa hivyo katiba mpya iendelee kufanya hivyo.

Vile vile polisi akishuku mtu, mtu yule achunguzwe polisi kwa masaa manane, ikiwa hakuwa na hatia mtu yule kwa masaa hayo aachiliwe.

Passport: tusiwe na vikwazo vya kutolewa passport, ati mpaka birth certificate za manyanya na mababu, hapana. Msingi ni mama na baba. Kitambulisho cha baba na mama utosheleze kwa passport kwa Katiba hii mpya. Katiba ya zamani, mambo ya zamani, tuwachane nayo.

Machiefs wasichaguliwe kwa kura: Ikiwa watachaguliwa kwa kura basi nidhamu ya machief itaanguka. Chifu ikiwa atachaguliwa kwa kura kwa hivyo atakuwa tayari mwanasiasa na hatakuwa na dhamani na ataanguka cheo. Kwa hivyo mimi maoni yangu naonelea machief wasichaguliwe kwa kura waandikwe na serikali. Kama vile tunavyoendelea kwa Katiba hii tuko nayo.

Lingine ni kwamba maeneo yetu ya Dondori tupatiwe wenyewe ile Kenya dhamani yetu iliyoweka maboya iondoshwe mara moja kwa Katiba hii mpya, ili wakulima wetu waende kule kwenye mazao. Hapa tulipo sisi, hakuna mazao kwa ukulima wetu. Dondori ni ardhi bora kwa watu, wetu rutuba kubwa iko hapo, na ----- imetuwekea maboya, na maboya kwa katiba mpya isiwe ikiendelea, iondoswe mara moja. Jambo la mwisho ni kusema: wavuvi, wa coast wawe na haki kama vile wavuvi wa sehemu zingine walivyo na haki. Wavuvi wetu wa coast hawapatiwi msaada wala mikopo. Kwa hivyo Katiba mpya ipitishwe na wavuvi wetu wa coast misaada, mikopo, wapatiwe ikiwa ni kweli ninavyo sema maana napenda kusema ukweli. Nafikiri nitakomea hapa, naambia kwaherini.

**Com. Mosonik :** Asante sana councillor. Kwanza tungependa kuwaomba wote ambao wamekuja kwa kikao wajandikishe nje hapo, hata kama hawapeani maoni. Kwa ajili mwishowe tutataka ku-report kwamba watu wa Lamu East wa Faza, nambari yao ilikuwa ni ngapi? Walikuwa na hoja kusikiliza na kutoa maoni kwa tume. Kwa hivyo mjiandikishe please. Sasa kusema kuhusu Tume, Councillor akasema ameona Tume nyingi zimekuja na kwenda. Tuna imani kwamba hii ni tume ile ya wananchi wenyewe, imeundwa na bunge, kuyasikiliza maoni na kuandika Katiba mpya. Kwa hivyo tuna imani kwamba yale maoini mtayatoa kwa tume hii hayatapotea bure, tuna imani. Haya, please, Bibi Bakari wa Bunoa Women Community. Na yeche ana memorandum atatupea mwishowe.

**Bibi Bakari :** Asalaam Aleykum, mimi jina langu naitwa Bibi Bakari Ali kutoka Tchulwa location na nawakilisha wanawake wa Tchulwa. Nitaanza na Haki za akina mama – wanawake wasibaguliwe katika kazi. Mwanamke wa Kisamu ambaye ni mfanyakazi wa serikali aruhusiwe akae eda miezi minne na siku kumi nyumbani, na alipwe mshahara wake kama kawaida. Mume akiachana na mkewe achukuliwe hatua au alazimishwe atunze watoto kwa mahitaji ye yeyote kama: chakula, elimu, matibabu na nguo. Haya, mume achukuliwe hatua serikalini iwapo atampiga mkewe. Mama asipokonywe watoto pindi baba anapomtaliki mkewe. Kunajisiwa kwa wanawake ambayo ni raping: Mtu ye yeyote mwenye kumnjisi mwanamke ahukumiwe

adhabu kali wala hakuna faini. Kuna wengine maanaka ni matajiri wataweza kutoa faini Kesi ya kunajisiwa iangaliwe au izikiliswe na askari mwanamke, hatutaki askari wa kiume. Mlalamishi asitishwe na wala asidharauliwe mahakamani.

Haki za watoto – watoto waelimishwe kutoka shule za mzingi mpaka mwisho. Iwe ni lazima kwa akina mama. Mama ambaye hatamsomesha mtoto wake au ambaye hatamuelimisha mtoto wake, achukuliwe hatua serikalini, na yule mtoto pia achukuliwe hatua serikalini. Elimu iwe bure kwa watoto. Matibabu yawe ya bure kwa watoto, tunasumbuka sana sisi huku. Watoto wasiozeshwe wakiwa wadogo. Mama yejote au baba yejote atakayeweza kufanya hivyo achukuliwe hatua serikalini, na adhibiwe vikali sana. Kwa sababu ni matatiso sana huku Lamu. Watoto wasifanyishwe kazi wakiwa wadogo – under age -. Mtoto wa kike na wa kiume waelimishwe sawa. Haki za watoto, wanaobandikwa mimba wakiwa wadogo, sikilizeni vizuri sana. Mtu yejote mwenye kumtia mtoto mdogo mimba alazimishwe aozwe. Kisha, ingine, amtunze mtoto kwa mahitaji yoyote baada ya yule mtoto kuzaliwa sasa, amtunze kwa mahitaji yejote muhimu: nguo, chakula na matibabu, mpaka afikishe miaka kumi na nane – 18 years.

Haya, ummasikini wa akina mama - namna ya kuondoa ummasikini. Akina mama wasaidiwe katika makundi ili wajiedeleze. Akina mama wapatiwe mikopo katika vikundi ili wajiedeze. Akina mama wahusishwe katika kazi mbali mbali.

Haya, watoto mayatima hasa walioachwa na mama zao kwa sababu ya ukimwi: serikali ichukue jukumu kuangalia mayatima kwa chakula, elimu, matibabu na nguo. Serikali iwajengee mahali pa kuangalia hawa watoto mayatima.

Wajane – wajane wenye ukimwi wahurumiwe, wapewe matibabu, chakula na nguo.

Haya, ndoa ya lazima – Mwenye kumuza mtoto wake kwa lazima ahukumiwe kisheria, yaani hatutaki ndoa ya lazima. Ndoa ya lazima isiweko kabisa.

Bunge – Viti nya maluu nya wabunge na ma-councillor wapewa wanawake. Kwa sababu kule bungeni tayari wanaume wametuzidi. Kwa hivyo viti hivyo twaomba kama wanawake wapewe nani, wapewe wanawake.

Uwazi na uwajilikaji – wanawake wawekwe mstari wa mbele kujulishwa mambo yanaoendelea serikalini na majumbani. Mtu wa kwanza kujulishwa awe ni mwanamke.

Tabia ya kuwanyanyasa akina mama katika mijji: Mwanaume yejote yule atakayempiga na kumjeruhi mwanamke, achukuliwe hatua serikalini.

Na Katiba iandikwe kwa lugha ya Kingereza na Kiswahili. Katiba ifundishwe mashulenii ili watoto wajue haki za nchi yao. Ma Asalaam.

**Com. Mosonik :** Halima Mukhdhar wa Ndeleni S. H. G.

**Halima Mukhdhar :** Salaam Aleykum, wananchi mlionhudhuria hapa nyote. Ni mimi Halima Mukhdhar kutoka Tchudwa na kikundi changu ni Ndeleni self group. Sina mengi isipokuwa, naakilisha kikundi changu kutoka Tchudwa. Naomba tume iongezewa muda kwa sababu kuna sehemu fulani ambazo hazijafikiriwa kufundishwa kwa sababu zisoweza kuepukika upande wa kifedha, upande wa security. Tunaomba tume ituongezee muda wa kufanya kazi hii. Kwa hivyo sina mengi. A salaam Aleykum.

**Com. Mosonik :** Bakari Bunu. Bakari Bunu please.

**Bakari Bunu :** Salaam Aleykum : Mimi maoni yangu ni juu ya mnyonge. Mnyonge kupata haki ni mwenye nguvu kupenda.

Kwa hivyo ningependekeza serikali iwe na haki, ili iweze kuchunguza haki za wananchi kisawasawa. Samahani, nitakaosema ukweli ukijikiri uwongo hujitenge. Ningependekeza kwamba serikali iwe ya ukweli. Wakati wote itakapokosa ukweli sheria nayo haitakuwa kisawasawa. Kwa sababu vile inatuletea udhaifa sisi wanyonge, wale wanao nguvu, serikali haiwezi kuangalia. Ningependekeza kwamba wanyonge waweze kupatiwa haki kisawa sawa. Hata ni heri kuangalia wanyonge zaidi kuliko wenyewe nguvu.

Lingine, ningependekeza kuhusu upande wa ma-headmen. Ma-headmen ni watu wenye jukumu, ningependekeza serikali iweze kuwapatia malipo angalau wahamasike ili nao waweze kutumikia nci sawa sawa.

Lingine – ningependekeza baraza la wazee wa kijiji watachaguliwa na watakuwa wakipata malipo nao kwa kwenda kushugulikia wananchi. Kama tume ilitolewa na wanalipwa na wananchi, na wazee wa kijiji nao walipwe angalani kitu kidogo cha kuwainua mgongo.

Kitu kingine kuhusu vitambulisho, ningependekeza ipitishwe kwamba: kila moja anaweza kupata kitambulisho katika Division yake, na anaweza kupata passport kulingana na wilaya yake, bila kupitia mahali pengine. Wilaya iwe inashughulika na mambo yote. Na pia isiwe na mivutano ama karatasi ya kuulizwa nyanya yako na babu yako. Kwa sababu wao wengi hawakuwa na makaratasi hayo, wamefika hivyo hivyo, sasa ukiuliza karatasi ya mzazi na mzee hakuna. Kitosheleze kitambulisho cha baba au mama, mambo yote yawe yatatimiya.

Ningependa vyama vya siasa viweze kuwekwa kwa mpango, isiwe ni holela. Kwenda kuwekwa kama vyama ni vitatu au viwili.

Pia ningependekeza wabunge wasiwe wanao uwezo wa kupitisha mishahara yao wao wenyewe tu. Ningependekeza iweko tume ya kuchunguza mishahara ya wabunge kikamilifu. Kwa sababu wale watu wanaenda wanakula sisi wanyonge, mishahara yao ni minono (inaudible) Wanakula miaka mingi sana, huduma inaharibika.

Pia ningependekeza Rais aweze kuongoza nchi kwa miaka miwili miwili, yaani miaka kumi isizidi, ili wengine nao wawezekupata nafasi, kujing'ang'ania kitiki kwa Bunge.

Pia ningetia nguvu Kadhi mkuu achaguliwe na viongozi wa kidini na ma-imamu, tena Kadhi awe ameelimika kwa elimu mbili - - ya kidini na ya kidunia.

Na pia ningependekeza Rais asiwe juu ya sheria wakati wowote, awe nani awe mtu wa kutumikia na akikosa awe ni wa kurudiwa.

Na lingine ni udhaifu wa rumande watu wakiwa katika rumande miaka ishirini, miaki thelathini, kwa hivyo yejote atapatikana na hatia achunguzwe. Ikisikika ana kosa ashitakiwe ajue amefungwa. Lakini, kuwa rumande kwa miaka mingi, nakutolewa maisha yake, naomba ile sheria iondoke. Nafikiri kuna wengi ambao wanataka kukaribia (inaudible)

**Com. Mosonik :** Asante. Tafadhalii ujiandikishe. Na sasa Bwana Mohamad. (inaudible)

**Mohamed Kassim :** Salaam Aleykum. Mimi jina langu ni Mohamed Kassim, nimekuja na memorandum kutoka kwa kijiji cha Chintu na vile vile nitakuwa na maoni yangu maalum. Maoni yangu maalum ni kwanza kutoa shukrani kwa Tume ya Katiba mlio hapa kutushughulikia kwamta ni watu watoka mbali, na serikali imeuliza ninyi mje hapa. Pili natoa hoja yangu maalum kuwa ikiwa tume imetoka mbali na serikali imekuwa jukumu kubwa kuja huku, yaani yale maoni ya wananchi yote yaandikishwe. Yale ya kila mwananchi atasoma vile Katiba ---onyeshwa katika nchi ya Kenya na ikiwa ni ku---bure---Lakini kila mtu. Maoni yangu mengine ningependa kuzungumza kwenye Tume ya Katiba mpya, chochote kuwa kwamba kimetengenezewa na binadamu, huwa haikufaa yaani kuharibika au kuwa kizee. Basi ningependa pia muone kwamba udhaifu wowote ambao hapa tumezungumza pia tume hii irudie kwa wananchi ili ichukuwe maoni kuhusu mambo yale yanaoendelea.

Katika maoni ya wale wengine, ningependa kuhusu mambo ya kitambulisho tusibaguliwe, yaani sisi tunabaguliwa sana. Kwa sababu kama ninavyo sema hivyo kama mimi hapa niko na miaka takribani, karibu hamsini. Na ndivyo sawa nikitoa kiufupi Mpeketoni ilikuwa mbali. lakini leo inawezekana kuingia mtu hapa kutoka Mpeketoni leo hii, akanisahihishiya mimi urahia wangu (inaudible). Kwa hivyo ichukuwe jukumu sisi tukitaka kitambulisho huku kwetu kuwe na taratibu mzuri na kuwa, asiwe ni mpaka mtu mgeni kumsahihisha mwenyeji, ni mwenyeji kumsahihisha mgeni. Kwa haya machache nafikiri nitapeleka memorandum yangu hapo.

**Com. Mosonik :** Mwana Amina Ali,

**Speaker:** Heavy Lamu dialect.

**Mwana Amina Ali:** Salaam Aleykum, mimi Mwana Amina Ali ----- Natummaini Tume itu fanyie kitendo maana yake siku sote hizi husema, kitendo hatuoni. Lakini dalili ya mvua ni kiwingu. Basi kwa hivyo ndio tunataka lile tunenalo tufanyiwe. Na sisi wanawake tuko nyuma sana. Twakataka tuendezwee nasi, mume akinywa mawili nasi tunywe moja. Kwamba tuna vihondo hapa nchini, tuna hari waume wetu hawana kazi, lakini hatuna maendeleo yoyote sisi. Tukitaka mikopo hatupewi, tukitaka deni kwa matajiri, watatupa? Hata muda wa kuvuna mwanaao asimame na punda (inaudible) ndio aweke kikapuni kwako. Basi kwa hivyo twaomba nyinyi serikali ituangalia na sisi. Hatujasomesha watoto wetu, wanawake kwa waume, tunawapeleka makoleji lakini (huringa kama vya yati) hawana kazi yoyote. (Na ikitokea kazi, twasikia mtakucha kupangwa usiku tuhaya hata tunge (inaudible) mtu sub chief na chief wake (inaudible) chora sini, tukimwangilia ni ntu Amu, tukimwangalia ni ntu mwingine hatusemee lolote sasa mwenye ratini hafanye yake na mwenye kizingitini kazi na mwenya ya bogi naya akapate sehemu kwa hivo asalaamu aleykum.) dialect.

**Com. Mosonik :** Okay, Mohamed Ali M Kwangazini, una memorandum?

**Mohamed Ali Mohamed :** Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu. Nashukuru Mwenyezi Mungu kunipatia nafasi kama hii, kwa wakati huu wa leo, kuwa mbele ya Makamishna na wazee wa vijiji vyote hivi. Jina ni Mohamed Ali Mohamed. Ni kupendekeza maoni ya wavuvi wa asili. Baada ya wavuvi wa asili kukaa chini, kupewa nafasi hii ya kutoa maoni yao, walionelea makubwa ni katika mali ya asili, ambayo ni sehemu imewabana zaidi katika Katiba iliyopita ya Kenya ambayo tuko nayo. Katika Katiba hiyo mali ya asili yalikuwa ni mali ambayo yako mikononi mwa serikali. Imemfanya mvuvi au mwanamke wa sehemu hii kuwa na hali ngumu ya kimaisha, kwa vile mali haya yalimilikiwa na (inaudible) serikali. Kwa hivyo mapendekezo yao ni kwamba, mali ya asili yawe mikononi mwa jamii iliyo karibu, ambayo ni ya sehemu hiyo. Kama vile maji, vilivyomo ndani ya maji vimilikiwe na jamii ya sehemu hiyo. (introduction)

Wananchi wenyewe waunde kamati ya kusimamia mazao na mapato yao. Ushuru wa mapato wa serikali na mitaa ziondoshwe kabisa katika Katiba mpya.

Tano, vikwazo upande wa fishery juu ya aina ya vifaa vya kuvuliwa samaki viondoshwe kabisa na Katiba mpya. Katiba mpya itoe vifaa muhimu vinavyo patikana kusaidia wavuvi popote walipo. Jamii yenyewe iwe na uhuru kulinda mali ya asili. Jamii iwe na uwezo wa kuhifadhi mazingira yake. Katiba itoe mafunzo ya uvuvi kila mwaka katika wilaya zote nchini. Katiba itoe misaada ya kifedha kwa kusaidia wavuvi. Asili mia themanini na tano (85%) ya faida inayopatikana kutoka bahari inayopakana na jamii fulani, wapewe wenyewe. Paki zote ambazo ziliwekwa na Katiba iliyopita, Katiba mpya iondoshe. Na paki hizo

ziwachiwe wenyewe, jamii. Katiba mpya pia iwe ni ya kumwachia mwananchi kuweka mzingira na kuhifadhi mazingira, sio wageni kuweka mazingira na kuhifadhi mazingira.

Kwa upande wa Rais: napendekeza kwamba Rais asiwe juu ya sheria kama Katiba iliyoko saa hii, imefanya Rais kuwa hivyo. Kwa hivyo Katiba inyoafwatia, namsihi msirudie kosa lile. Hapo nimefikia mwisho.

**Com. Mosonik :** Sasa tutamsikiliza MBwama Women Group

**Batitu MBwama :** Asalaam Aleykum, Mimi jina langu naitwa Batitu MBwama kutoka Siu naakilisha Siu Women Group. Kunajisiwa (raping case): mume anayenajisi mtu, mtoto ama mukubwa, ahukumiwe kifungo cha maisha, ama akatwe ume wake. Atakaye najisi mwanamke au mtoto mdogo ahukumiwe kufungwa kifungo cha maisha.

Haki za watoto: watoto walelewe kibinadamu, na wapewe elimu ya kutosha, wala wasitupwe wakawa chokora. Watoto waelimishwe elimu, desturi na mila za dini zao. Serikali ichukue jukumu ya kuwalinda watoto waliotupwa na kuwachukulia hatua waliotupa watoto. Serikali itambue watoto waliotupwa - - kuwalisha na kuwasomesha elimu - - kama watoto wengine.

Elimu: iwepo shule za kitaifa, pia vyuo vikuu pwani ili kurahisisha gharama. Elimu ya shule za mzingi na wanaopita mitihani wasomeshwa bure. Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu.

**Com. Mosonik :** Hussein ----naye ni chief, please. Atoe maoni yake.

**Shibala Mohamed :** Asalaam Aleykum, kwa majina mimi ni subchief Shibala Mohamed, kutoka kata ya Mulimwali. Mimi nitatoa maoni yangu ya binafsi. Wanakamishna or Commissioners ninapendekeza swala la mishahara. Nasikitika kwamba hali ya uchumi ya nchi iko juu sana na mishahara wanaopatiwa wafanyakazi ni midhaifu sana. Mfanyikazi wa chini anapata mshahara wa 1,800/= ambazo zatosha kwenda Lamu na kurudi. Kwa hivyo naomba serikali iunde Katiba mpya ya kwamba mishahara iwekewe tume maalum, na kiwango cha chini kiwe ni elfu kumi. Vile vile Katiba mpya iundwe kwamba wabunge, wajumbe, wasijiwekee mishahara watakayo, ila iwekwe sambamba na viumbe wote katika ulimwengu. Twende madaraka fulani lakini wakati huu, tunasukumika na wajumbe wa Bunge pamoja na mawaziri. Wewe na mimi kama machief tunafanya kazi nydingine yejote, twende sambamba kiasi fulani lakini siyo laki tano - - machief hata hiyo tano hawapati.

Kitu kingine ambacho ningependekeza kwa Katiba mpya iundwe ni kuhusu habari ya magereza, hususana kwa waislamu. Wakati wameenda korokoroni au wanaenda kwenye jela, hawapatiwi haki zao za kiibada. Kwa hivyo tunataka Katiba iangalie. Wakati mkubwa atawekwa gerezani au atakaa katika rumande, awe anapata haki zake za kiibada, apatiwe nafasi kama sisi aweze, kumwabudu Mwenyezi Mungu.

Kitu kingine napendekeza Katiba iunde ni kuhusu cheti cha kusafiri (Passport). Ningependekeza passport kwa wanakenya wote bila kuangalia kabilia, rangi au dini. Ipeanwe kama kitambulisho. Imekuwa nitatizo sana kwa Waislamu kubaguliwa kwenye kitu kama hiki.

Sasa ningependa kupendekeza juu ya uchaguzi. Nikipendekeza Katiba ya uchaguzi unao kuja masanduku ya uchaguzi yawe yenyeye kuonyesha (yaani transparent). Hatutaki masanduku yenyeye giza hapa na kutuhadaa. Vile vile uchaguzi utakapofanyika, kura ihesabiwe kwa kila kituo. Wale ma-agent wanasmamia mambo ya kupigwa kura, wajue kile kituo kura ngapi ziliandikishwa na ni kura ngapi zimepigwa, hatimaye wahesabu siku hiyo, hiyo, hapo, hapo. Mshindi wa uchaguzi ikiwa atakuwa ni councillor, au ni mbunge atangazwe kule ambapo atapata asili mia hamsini (50%) za kura zilizopigwa katika eneo lake. Si mtu apewe kura mbili au kura moja awe kingoz, i hajakuwa kiongozi huyu. Kiongozi ni aliyepata kura asili mia hamsini (50%) na kura zote zilihesabiwa kama aanguke niza ubunge au za ucouncillor. Na ikiwa hawakufikia hivyo, basi mshindi wa kwanza na mshindi wa pili warudie round nyingine. Hapo hapo kwenye viongozi wa kisiasa, na hata viongozi wa kiutawala: ningependekeza Katiba itungwe kwamba mjumbe mbunge, councillor, hata chief na mfanyi kazi yejote wa serikali lazima awe amefikia umri wa miaka 35. La si hivyo hajadhubutu kuwa kiongozi wa kisiasa.. Nilikuwa na mengi yu kuzungumza, lakini tulikuwa tukiomba hapo mbele ya kwamba tusirudie rudie ili tuweze. Sababu mengi ningetaka kusema wenzangu wameyasema. Kwa hayo machache nasema asante.

**Com. Mosonik :** Ningependa kuuliza ni nini amesema, kuhusu nini? Umesema mwenzako amesema, lakini kuhusu nini?

**Shibala Mohamed:** Yale yalikuwa ya kuzungumza ambayo wenzangu amezungumza ni juu ya wajibu wa Kadhi, kwa makamu na machief kadhi, mambo ya environment, yaani mali ya asili – natural resources, na mambo mengine ya wajumbe kuwa na majukumu ya kujinyakulia ile mishahara wanaotaka wao. Asante.

**Com. Mosonik :** Swala lingine umesema kuhusu eneo ya waakilishi bungeni ama council, kwamba wawe na kura asili mia hamsini (50%) na kuhusu Rais wa nchi?

**Shibala Mohamed:** Hata hivyo Rais wa nchi vile vile mpaka apate asili mia hamsini (50%) za kura zote nchini. La, si hivyo arudiwe.

**Com. Mosonik :** Nataka kuuliza tena, kama ulisoma kijitabu - - maswala na maswali, kuna swala letu: Je tuendelee kuwa na kanuni ya asili mia ishirini na tano (25%) ya waakilishi katika anga mikoa mitano, katika uchaguzi wa Rais au la?

**Shibala Mohamed:** La, hatutaki hivyo. Tunataka Rais apate asili mia hamsini za kura zote nchini. Habari ya mikoa iondoke. Sababu mikoa inaenda kikabila. Kuna mikoa mingine, kuna makabila, kama Central, nitatoa mfano, ni Wakikuyu watupu. Kama Rift Valley nao ndivyo hivyo hivyo. Naweba kusema ni mbari moja - - Mkalenjini na Mnandi. Sababu ya kusema ni

mbali moja, wakati mwingine unaona wote ni kitu kimoja. Kwa hivyo tutaenda kwa asili mia hamsini (50%) kura za nchi yote.

**Com. Mosonik :** Okay, asante.

**Shibala Mohamed :** Sawa, nataka kuongeza kidogo. Kitu kimoja kama nimepewa nafasi ndio niseme. Kitu kuhusu uraia. Napendekeza mwanamke na mwanamume wa jinsia zote wawe ni raia bila kuzingatia jinsia yake. Kitu kingine mtoto aliyezaliwa na Mkenya hima mke au mume Katiba mpya ampati uraia. Vile vile ningependekeza vitu vitatu viwe vinamfanya mtu ajulikane ni Mkenya. Na hizo ni mtu wowote, si—kuzaliwa, yaani cheti cha kuzaliwa, akifika umri wa miaka 18 akipewa kitambulisho apewa Passport, wakati wowote tukitaka kusafiri ndio tunaweza kufanya usafiri wetu kwa urahisi, bila kwenda kukitishwa karatasi ya babu, sijui ya nyanya, (inaudible). Kwa hivyo mtu kutambulikana ni Mkenya, akizaliwa tu awe anapata cheti cha kuzaliwa na wakati atakuja kuchukua kitambulisho, pia akitaka Passport wakati huo apewe. Hivi ni vitutatu ndio vinaweza kufanya mtu awe ni raia wa Kenya.

**Com. Mosonik :** Na kama raia anaye mtoto amezaliwa kwa Balozi wa Ufaransa ambaye anafanya kazi Kenya, azaliwe king Fani hospital na apewa birth certificate?

**Shibala Mohamed:** Sawa, hiyo vile vile napendekeza ya kwamba ikiwa Mkenya yupo nje kikazi, kazi ya serikali au kazi yake binafisi. (Kama kwa mfano nina ndugu zangu wengi wako Saudia saa hizi wanafanya kazi. Ni Wakenya na wameoa wana bibi zao, na akizaa, kama baba na mama wana kitambulisho cha Kenya, aende kwa office ya Balozi vile, a-register kwamba mtoto wake amezaliwa na ubalozi wake umuakilishe kama unavyomuakilisha akiwa hapa nchini). Kwa hivyo anaweza kupata uraia wa nchi hii.

**Com. Mosonik :** Sio kukusumbua wajua wewe ni Chief, na wewe ndio kiongozi. Sasa ninauliza kama Balozi wa nchi ya ng' ambo anafanya kazi area hii ya Faza, na mtoto azaliwe kwa hii health centre na apewe birth certificate, ndio awe raia wa Kenya?

**Shibala Mohamed:** Hapana, mtoto wa Balozi wa kutoka nchi ya nje, asipewe uraia mtoto wake akizaliwa hapa. Ubalozi wake, office yake ya ubalozi hapa nchini Kenya impatie, cheti cha kuzaliwa katika nchi yake. Kuna lingine?

**Com. Mosonik :** Hapana, ni sawa, ni sawa kabisa. Yaani tulitaka tu kujua kwamba, birth certificate, ubaya wake ni kwamba haionyeshi uraia. Inaonyesha mtu fulani alizaliwa, mahali Fulani. Na yeze anaweza kuwa ni mgeni akizaliwa nchi hiyo. Ndio pengine inasemekana haitoshi. Kwa ajili mtoto wa Philipian mama yake akimzaa Nairobi, si anapewa birth certificate kwamba, alizaliwa kwa hospitali? Lakini hiyo sikumaanisha yeze ni raia wa Kenya. Pengine hiyo ndio shida.

**Shibala Mohamed:** Ndio hiyo, nasema hivyo, basi narudia tena tungetengeneza nchi yetu, kwako Kamishna na hata kwa

wenzangu. Ikiwa balozi, yuko hapa either ni wa Canada, Ujerummani, awe mtu mwininge yejote, ikiwa atazaa hapa Kenya kwa hospitali, ikiwa ni Aga Khan au ni Kenyatta, wakati anataka kupata cheti chake cha kuzaliwa, ubalozi wake unaomuakilisha hapa nchini, umfanyie mpango ya kupata cheti chake cha kuzaliwa kutoka kwa nchi yake.

**Copm. Mosonik :** Asante, asante sana. Next tutakuwa na Imam Maalim Abud.

**Imam Maalim Abud:** Salaam Aleykum wa Rahamatulilahi Wabarakatu. Jina langu ni Maalim Abud mtu wa Kizingitini nikiwa kama Imam wa Jamia Mosque, Kizingitini. Maoni yangu au maoni yetu pamoja na wale ambao tunaswali pamoja katika Msikiti, ni haya yanayofwata:

One, Ni kifungu cha Kadhi – Kadhi asichaguliwe na Kadhi mkuu, au asichaguliwe kwa sababu amesomea shule, kama wanavyochaguliwa sasa. Mtu akiwa na cerfificate ya shule ndio anachaguliwa kama Kadhi kwa sababu yeye amemaliza secondary school. Kisheria, maadam yeye anakuja kusimamia Uislamu, ni mpaka awe amesomea Uislamu, awe na shahada ya kwamba ameitimUislamu, ndio apewe kazi kama Kadhi. Pili Kadhi huyu huyu, awe na sauti kama Judge. Kwa sababu zikija kesi kwake awe anahukumu kesi hizo kama Judge na apewa cheo cha Judge kama judge wengine.

Kadhi Mkuu: Kadhi mkuu awe ndiye Judge mkuu katika Uislamu. Apitishiwe Kadhi Mkuu, awe kesi zote zitakazo washinda makadhi, zipelekwe high court na high court yake iwe mkubwa wake ni Kadhi Mkuu ndiye mwenye kusimamia. Sio itolewe kesi kwa Chief Kadhi ipelekwe high court kwa kurundika kipi sasa? Bado hatujapewa uhuru kamili. Ikiwa kesi imeshinda kwa Kadhi Mkuu hakuna mahali pengine pa kupelekwa. Kama inayo shindi katika High court, huwa ndio basi. Kwa hivyo kesi yoyote inayoshindwa kwa Chief Kadhi iwe ndio umemushinda hio, hakuna mahali pengine mtu anaweza kukimbilia. Isitolewe kesi kwa Chief Kadhi ikapelekwa mahali pengine, kwa sababu ni kesi ya Uislamu, ibakie pale pale kwa Waislamu wahukumu Chief Kadhi kulingana (inaudible). Halafu Kadhi Mkuu, kuchaguliwa kwake, kuchaguliwe na kamati za maimamu pamoja na wanavyuoni, asichaguliwe na serikali, kama kibaraka cha serikali. Kwa sababu serikali huchagu ni nani maziwa lala, nimuweke mahali hapa, nipate kuangalia Waislamu. Achaguliwe na Waislamu wenyewe. Waislamu ndio watakaomueka, mtu ambaye anafaa, kihakika huyu hufwata sheria za dini na kuturudishia mambo yetu.

Jambo Lingine ni katika mambo ya stakbadhi – Vitambulisho, Passport na Birth Certificate. Mambo haya sisi wa Pwani twabaguliwa, hatupewi sisi wa Pwani kama wanavyopewa watu wa Bara. Mtu wa Bara akishajulikana jina lake ni Onyango, au ni Katana au ni Karithi au yeye ni Njuguna, basi tikitambulisho za babake na mamake, chatosha yeye kupata kitambulisho chake. Apewe kitamblisho chake kwa sababu ya mama yake na baba yake. Sisi Waislamu, ikiwa jina lako ni Mohamad au ni Asmani au ni jina lolote la Kislamu, halitoshi wewe kuwa na kitambulisho cha baba na mama, mpaka uongeze na mambo mengine. Tena, uchunguzwe kama wewe ni mkweli ama murongo. Tusiwekwe mahali pa ubaguzi, sisi na watu wa bara, zote ni Wakenya, tukapewe sheria za Kenya kwa ujumla kwa pamoja zote. Lile ambalo ni wajibu  
nipewe lini na Njuguna iwe hivyo hivyo. Ikiwa Njuguna ana haki ya kupewa kitambulisho kwa kitambulisho cha mamake na

babake, na mimi Mohamad nipewe hivyo hivyo, sio kwamba mimi nilaliwe.

Lagine, tofauti ya mambo ya kupewa kitambulisho kwa upande wetu. Tumelazimishwa tutafute na vitambulisho (yaani katika kutafuta passport) lazima kuleta Birth certificate za wazee wetu waliokufa. Haya ni makaratasi ambapo watu wa nyuma walikuwa hawakushugulika nayo. Kwa hivyo kifungu hiki cha kutafuta Birth kiwe kitaondolewa, ikiwa ni Birth yangu mimi mwenyewe, au ni birth certificate za babangu na mamangu, kupewa Passport bila kuambiwa nilete birth certificate au ulete certificate kwa mambo marefu, ambapo mtu mwengine iko rahisi kupewa, sisi watu wa Pwani, kubaguliwa.

Mambo mengine ni ya uvuvi. Uvuvi, huku Pwani upande wetu, ndio uti wa mgongo wetu. Ndilo jambo ambalo tunategemea, hata sisi watu wa Lamu. Mavuno yetu yote hutegemea mambo ya uvuvi. Na ni eneo kubwa au ni watu wengi sana wanaokuwa upande wa Pwani, wa Lamu kuliko watu wa bara wanavyokuwa. Lakina ajabu ni kwamba, kuna tofauti kubwa sana watu wa bara wanaovua bara, wamekuwa matajiri. Sisi tangu jadi wazee wetu wamekuwa wakivua na mpaka leo wanavua, na ndio maskini tu. Kwamba serikali yawasimamia watu wa bara. Ikiwa juu ya mikopo ama mahali pengine katika nchi zingene, huku watu wa Pwani tumelaliwa. Serikali yawatafutia masoko kuuza mazao yao yaktoka pwani. Sisi tuaambiwa tafuteni wenyewe kama hamna mahali pa kuuza laleni, mfe njaa. Tuangalia samaki wanaotoka Lake Victoria ni samaki kama shogo, kilema, na kama samaki mwengine. Si kwamba ni samaki wa maana mpaka akapata soko kubwa kushinda sisi. Samaki wao ni kama hawa wetu tu. Ni kama shoko, samaki wa mamba, wale hutolewa wakatengenezwabidhaa zikasafirishwa waenda kuuzwa nje. Je, sisi hatuna samaki hao wa kwenda kuuza nje? Tunao, lakini serikali haitaki kutuangalia sisi huku. Kwa hivyo tuwekwe usawa, kama mtu wa bara na mtu wa Pwani, tuwekwe usawa, pamoja kama Mkenya. Serikali isiangalie upande mmoja, iangalie pande zote kwa usawa. Kama vile Katiba imeambiwa itungwe mahali (kote ndio mpaka tume leo ikaja hapa kwa sababu imejua kwamba ichukuwe maoni) kwa usawa. Kwa hivyo, na usawa utimike na kwa njia zingine, si kwamba shauri ya maoni tu. Kwa sababu ya maneno (inaudible ) tuwe kwa zote.

Jambo la mwisho – Kuna kifungu kingine nimesikia hapa kikizungumzwa kwamba mbunge achaguliwe, yule ambaye ni mzaliwa wa Kenya. Mimi nafikiri ya kwamba, la, sivyo hivyo. Kwa sababu maadamu ni Mwanakenya, amepata uwanakenya wake kwa njia yoyote, basi ana haki ya kusimamia mahali popote anapotaka yeye mwenyewe. Watakaoamua ni wananchi. Madamu ni mwanakenya kwa kujandikisha , kwa kuzaliwa, kwa ukoo, kwa njia yoyote, apewe nafasi aende kwa wananchi asombe kura. Wananchi wawe ni suluhusho, twakutaka au hatukutaki? Kwa sababu yeye ataenda kuomba kura kwa wananchi na wananchi ndio wataamua kwamba mtu huyu atatufaa au hatufai, akiwa yuwafaa, na serikali impinge mtu huyu asisimame, tayari wananchi wamedhulumiwa na serikali. Kwa sababu mtu anayefaa, kiongozi anayefaa, na serikali imemkataa. Kwan hivyo wasio wenyewe wananchi wachague mtu wanamtaka, wasiingiliwe na mtu mwengine? Wasalaam Aleykum warahamthulilahi wabarakanatu.

**Com. Mosonik :** Yusuf Omar, Yusuf Omar.

**Yusuf Omar :** Salaam Aleykum, mimi kwa jina ni Yusuf Omar, mkaazi wa Kizingitini location. Kwa hivyo maoni yangu mimi ya kwanza nayotoa kwamba, katika Kenya hii kuna mikoa mingi lakini tuna masikitiko ya kwamba, mpaka sasa hatujawenza kuwekwa pahali huenda kuwekwa nasi university. Tuna watoto hodari, mashujaa ambao akili zao ni kali mpaka tukakuwa university katika sehemu hii. Kwa hivyo naona Katiba sasa ijaribu ione serikali itufanyie na sisi hakuna university katika mkoaa wa pwani. Kwa sababu tayari tuko na watoto wanaotoka katika hii sehemu ya Faza, Kizingitini kwa mashule ya kitaifa, ambao wanatarajiwa kesho kwenda university. Sasa pengine hata mzazi hawezhi kwa sababu malipo yako magumu sana. Akili yake imesoma na (akina) inandibu fulani arudi kule alipotoka.

Maoni mingine ni kwamba: mpaka sasa sisi katika sehemu hizi zetu, kuna miradi fulani ambayo serikali yaweza kusaidia au mashirika yaweza kusaidia. Lakini masikitiko ni kwamba, wakati tunapoteza hatuwezi kuwa na kilio kingi, kwa kuwa sio watu wanatoka sehemu zingine ambao hawajui mazao huwa na faida gani. Kwa hivyo jambo la kwanza ni kuwa tupewe nafasi zetu wenyewe ili tuweze kujua nafasi zile zinapatikana kwa njia gani tuwe tukidumu. Kwa sababu ni hasara kubwa kwa mashine kama -----Majengo mtu anakuja kujenga, si kwao -----hasara ni kwetu. Kwa hivyo shirika halitusaidii, serikali itujalie. Lakini twaharidhika. Kwa majengo ----kwa hivyo nafasi hizi bado ziko ---mwenyewe.

Jambo lingine katika mashule haya tulio nao kama primary school, Serikali ilete waalimu wa kidini, wawe na nafasi ya kusomesha katika shule hizi, wakilipwa kama waalimu hawa wengine. Sababu ya kusema hivyo, kwamba kuna watoto wengine wanasoma shule baada ya kumaliza primary, kwenda secondary, ile elimu ndogo wako nayo ya kidini itapotea. Kila sehemu wawe na waalimu wanao wakusomesha wa serikali.

Jambo lingine kutiliya nguvu ni kuhusu mambo ya uvuvi. Leo hii Lamu district ndio nchi ya kwanza katika Kenya kwa uvuvi. Lakini leo hii utakuja kukuta kwamba samaki tulio nao katika baharini hatuna nafasi ya kwenda kuwaokota. Kwanza tumenyimwa vifaa nya kwenda kuvulia sehemu za mbali. Pili, hata tukiwa na vifaa nya kuvulia sehemu za mbali, tukishavua hatujui tutamweka mahala gani, na sisi hatuna system yoyote ya kwenda kuweka samaki au hutuna store yoyote ya kwenda kumuweka samaki. Lakini ajabu kwamba sehemu za bara kunazo. Kuna sehemu za soko ambazo zimejengwa ma-coldstore, serikali yawaleta mikopo, vifaa na ambapo watu wengi kwa uvuvi hawasumbuki. Samaki ambaye aitwa shogo au kilema, nafikiri ndio mbuta, na bahari kenyewe kafupi, kabahari ya Matiba.

Ikiwa sisi ni wananchi wa Kenya twafaa tupewe haki halisi ya Kenya kama watu wa bara. Tupewa msaada kama kama watu wa bara. Haki yenye kupewa Mkenya halisi, na twafaa tuhurumiwe kama yule mtu mwengine. Kwa hivyo ingekuwa muhimu zaidi kwetu kama eneo letu lina wavuvi. Hatuna kahawa, hatuna majani chai, hatuna hata hospitali hata ukashindwa na jambo lolote huwezi lakini akili tunazo. Lakini bara kuna majani, kuna kahawa, na kila mmoja ana haki ya kumiliki ardhi, hana haja ya vitu vyake (inaudible). Haya yametosha.

**Com. Mosonik :** Asante, Jumbe Kasim – Faza women Group.

**Jumbe Kasim :** Salaam Aleykum - Jumbe Kasim, nazungumza kwa niaba ya Faza Women. Haki za wanawake: Wanawake wa Kisamu tunataka Katiba ihudumie swala la wanawake walio ajiriwa serikalini wapewe likizo la mieze mitano ya eda, pindi tu wanapofiliwa na waume wao. Wanawake wa Kisamu wamelazimika kukaa muda wa siku arobaini baada ya kujifungua, kwa hivyo, muda wanaopewa kufanya kazi hiyo haitoshelezi huduma hiyo ipasavyo kulingana na dini kwa hivyo muda wanatoa sasa uongezwe. Wanawake wafanya kazi hawapatiwi nafasi ya kutunza watoto wao uchungani. Kwa hivyo nafasi ya likizo inapaswa iongezwe.

Ofisi ya kadhi iwe na jukumu la kuhukumu kikamilifu bila ya kupendelea upanda wowote. Kesi za mume na mke wa kislamu zipelekwe kwa Kadhi siyo katika mahaka usaidizi za kama hakimu.

Wanawake wawe na uwezo wa kumiliki ardhi. Zahanati na hospitali ziwe na vifaa vyta kutosha. Malipo ya hospitali yapunguzwe. Elimu ya afya isambazwe kikamilifu kivijiji. Wakunga wawe wanawake katika zahanati na hospitali za kislamu. Wanawake waruhusiwe kuvala mavazi ya kislamu katika mataasisi.

Watoto wahukumiwe na serikali ikiwa hawataki kusoma. Wasichana na wavulana wapewe elimu sawa.

Wazazi wahukumiwe vikali kwa kuwaoza wasichana wao mapema.

Wanawake watengewe viti bungeni kama asili mia thelathini na tano (35%). Ikiwa hapati kuchaguliwa, wapewe vitu maalum vyta ubunge na udiwani. Asante.

**Com. Mosonik :** Kasim -----

**Kassim Gaabe :** Kwa jina naitwa Kasim Gaabe, kutoka Tchundwa Location. Mimi nina maoni yangu binafsi.

Kwanza nilikuwa nikizungumzia kuhusu Kadhi. Isipokuwa imeguziwa na wenzangu hata miminitaguzia. Kadhi lazima awe mtu ambaye amesoma kote kuwili na amefaulu, siyo kuwa amesoma tu peke yake. Kwote kuwili namaanisha elimu ya kidini ndio ya kwanza na ingine ni ile tunanayo (secular education). Kadhi apewe uwezo wa kuomgalia matatizo ya waislamu yote, kwa sababu islamu si kuridhi, si kuo wala si kuachana. Yapo mengi sana, kwa hivyo Kadhi awe na uwezo wa kuangalia mambo yote.

Lingine ni haki, sisi paka leo hatujapewa haki ya kutawala.. Pia haki za kienyeji zikubalike kama haki kamili.

Lingine ni kuna maeneo ambayo yametengwa mfano ya shule, ya hospitali na mambo mengine ambayo jamii ipate kuyatumia.

Twaomba serikali itoe hati za kumiliki sehemu hii kwa haraka iwezekanavyo, ili kuzuia wale amba wenyewe kuvamia sehemu hizi amabazo zatumika mbeleni.

Pia kuhusu wanawake, nilikuwa na pendekezo hilo hilo wapewe ruhusa ya kutosha punde tu waume wao wamefariki ambayo sisi Waislamu hatupewi kuna baadhi ya wanawake wenzetu wamekosa kazi kwa mambo kama hayo, ambapo si haki kukosa kazi kwa mambo ya kufiliwa.

Lingine, kuna sisi wanaume baada ya mtu kutokana bibi yake, huacha watoto. Kwa hivyo twaomba katika katiba hii inapoundwa tuwe na kifungu kuwa mzazi wa kiume mwenye kutupa watoto ashitakiwe. Kwa sababu, hii ndio huleta mambo mengi sana mabaya kwa na watoto - - wakiwa hawasomi au wanapatikana kwa uhalivu.

Lingine ni kuhusu mambo ya upeanaji wa vyeti: kitambulisho, Passport, na karatasi ya uzazi. Hizi zitolewe pasi na masharti mrefu kuitia. Kwa sababu nikiwa mimi tayari niko na kitambulisho, si tayari ni Mkenya? Kwa nini mtu aniuilize kitambulisho cha baba na mama? Ina maana sikupewa hati kama hizo, basi si Mkenya. Ikiwa si Mkenya, kitambulisho nilipata vipi? Kwa hivyo hii serikali yenye we yajizua huku yajifunga huku. Kwa sababu wampa mtu kitambulisho kisha baadaye wamuuliza maswali mrefu, ina maana kwamba wewe kutoka mwanzo yamefanya makosa. Kwa hivyo kama mtu ana kitambulisho basi kitambulisho kitoshe, na apewe hati zingine bila masharti yeoyote.

Katiba mpya tunaomba ikifaulu, serikali yenye we ina mambo ya lazima yafanye kwa wananchi, na serikali yenye we hutoa ahadi na ikapitishwa kuwa jambo fulani lifanyike, lakini tu.(inaudible) Kwa hivyo wananchi wenye wapewe uwezo ili serikali pia ishatakiwe. Serikali inafaa kushtakiwa, ashatakiwaye si mtu tu amekosa. Mfano kama vitu muhimu kama: elimu, afya, maji, usalama, serikali lazima itoe. Kwa hivyo punde tukikosa haya serikali lazima ishitakiwa itoe huduma kwa wananchi.

Pia kuna shirika lililoundwa la Anti-corruption unit, lakini hili tunajua ofisi zake sana ziko Nairobi peke yake. Kwa hivyo twaiomba katiba mpya ikianza, hii unit pia iweko katika kila baraza. Kwa sababu mwananchi hufanyiwa dhuluma na mfanyakazi wa serikali, na akawa hajui mwananchi aende wapi. Kwa sababu polisi imefilisika, sasa utashtaki wapi? Na pengine ni yeye polisi basi hatuna pa kwenda. Kwa hivyo twataka unit ya Anti-corruption pia iwekwe hapa kama serikali imenidhulumu, niweze kwenda hapo unit. Lakini kuwekwa huko Nairobi, sisi wengine tunaumia huku. Kwa hivyo Anti-Corruption unit iwekwe kila location.

Kuhusu Bunge – Bunge letu twajua kulingana na katiba tuliyo nayo, Rais ndio atasema sasa Bunge liishe au liendele. Kwa hivyo hiyo hatutaki. Twataka muda amba uko tunajua, ukisomeshwa shulenii tunajua, muda ni wa miaka mitano. Kwa hivyo ubakie huo huo muda wa miaka mitano, likianza paka limalizike. Hatutaki Rais aseme Bunge miaka mitatu limeisha, au Bunge ni miaka sita au ni miaka tano. Kwa hivyo muda liowekwa, ukifika, Bunge limalizike.

Pia twaomba Bunge lenyewe likizungumza - - pengine ni watu fulani Nairobi huenda wakahudhuria wakasikiliza mtu ambaye yuko huku kwetu, pengine ni baada ya saa tatu usiku kusikia ‘Leo Katika Bunge’. Kwa hivyo twaomba sasa ma-radio na television zipewe uwezo, wakati Bunge likiendelea, mtu aliyeko Nairobi na mtu aliyoko hapa sasa naye pia asikie. Akiwa yuko Lamu au yuko Faza kwa TV yake aangalie Bunge vile lazidi. Kwa sababu hii yatupa sisi uwezo wakati wa kuhairishwa kwa Bunge, kwani tutajua ni serikali iliyo sawa au serikali ya matatizo. Kwa hivyo Bunge, likipendelea wananchi wenyewe wasikilize au waone.

Lingine kuhusu Wabunge – Wabunge ni wafanyakazi, ni watumishi wa raia, kwa hivyo pia napendekeza kuwa na wao wawe weko kazini kwa wiki nzima. Jumatatu mpaka ijummaa naye awe kazini kama kila mtu. Siyo ye ye aende Jummane, Jummatano, na Alhamisi, siku zingine aangalie mambo ya kumanga manga hapa na pale kupoteza wakati wetu bure. Wafanye kazi sawa sawa.

Twajua serikali huunda tume nyingi kama hii iko hapa leo. Utakuta mwisho, husikia Tume imemkabidhi kiongozi wa nchi, matokeo ya kazi waliopewa. Lakini kusikitisha, majibu yale kwa wananchi hayafikiriwi, wala wenyewe hawayapati. Kwa sababu wao wote Makamishna hawana ithini ya kutangaza matokeo ya kazi waliopewa. Kwa hivyo Katiba mpya twasema: Tume ikichaguliwa ipewe uwezo wa kutangaza matokeyo ya kazi waliopewa, sio Rais ndio atangaze, Tume yenye, mwenyekiti mwenyewe. Kama saa hii tuko na Ghai ndiye mkubwa wa commission, ye ye Ghai mwenyewe awe na uwezo kutangaza matokeo ya Tume, lakini sio Rais. Kwa sababu wezekano imemkashifu Rais, atatangaza kweli? Hata kama ni mimi zingetangaza, kwa hivyo mwengine pia itakuwa hivyo hivyo hahtangaza. Na pia hizi Tume zenyewe, usipokuwa tunashukuru kwa Tume ya Katiba imepitia njia mzuri, ya kupita kwa Bunge na kuiithinishwa na Bunge. Na twaomba na Tume zote zinazochaguliwa zipite kwa Bunge. Hatutaki Tume ichaguliwe na mtu fulani. Kwa sababu mwenye kuchagua, ni kama kumpa mtu sima, utampa mtu sima kila siku ajue huyu ukimpinga leo sima yako ataondosha. Kwa hivyo hatutaki mambo kama hayo. Tunakata Tume lichaguliwe na Bunge. Nafiki hayo ndio maoni yangu liniliyonayo, na twaombea, kile jambo tunesema liwe lenye kufaulu. Asante.

**Com. Ahamed Hassan:** Nilikuwa nimeombwa na Commissioner nijaribu kujibu lile swali ambalo huyo ndugu yetu amesema. Kwa kweli, ukisoma sheria ambayo imeunda hii Tume, haijasema ya kwamba itakuwa ni Rais atatoa habari ya report yake. Bali ni kwamba, Chairman, tukimaliza kufanya kazi, tutengeneze report, sheria inasema tutampelekea Attorney General, yaani mkuu wa sheria, ambaye atapelekeea Bunge. Hakuna siku ama mahali ambapo Rais anaitahitajika awe akipewa hiyo report, ama ye ye atakuwa akitoa hiyo reporti. Hii Tume ya kurekibisha Katiba sio kama ile Tume ya kawaida ambayo mumezoea, kama ile ya Njonjo ama zile zingine za tribal clashes. Hizo ni Tume ambazo Rais mwenyewe alikuwa amezienda. Lakini hii Tume imeundwa na Parliament, Bunge, na itareport kwa Bunge. Kwa hivyo usijaribu kufananisha hii Tume na hizo zingene ambazo Rais alikuwa amezitunga. Kwa hivyo msiwe na wasi wasi. Hii report ya hii Tume itakadhibiwa Parliament, Bunge, sio Mtukufu Rais.

**Com. Mosonik** : Kwanza tukimaliza kukusanya maoini, tunaandika report ya Katiba kulingana na maoni ya raia. Halafu hiyo report na ile Katiba tumeiandika, tunawasilisha kwa mkutano wa kitaifa – National Constitutional Conference, ambapo kutakuwa na watu kama mia-sita hivi. Wajumbe wote wa Bunge, waakilishi watatu wa kila wilaya, waakilishi wa vyama vyasiasia kama arobaini na mbili hivi, Makamishna wenyewe, na waakilishi tunaowaita civil society. Watu kama mia sita wajadiliane, na wasikilizane na wakubali report yetu na Katiba vile tumeiandika kulingana na maoni ya raia. Na kama hawatasilizana, tutarudisha report na ile Katiba kwenu kupidia kura ya maoni, inaitwa Referendum. Tutapiga kura kusema hatujakubali ama tumekubali. Halafu baada ya hapo inawasilishwa Bunge, vile mwenzangu ameeleza kupidia kwa Attorney General. Kwa hivyo tuwe na imani kwamba kazi tunaifanya ni ya maana. Okay. Councillor Badi Amir please.

**Councillor Badi Amir** : Salaam Aleykum wa rahamtulilahi wa barakatu. Jina langu ni Councillor Badi Amir, naakilisha area hii ya Faza.

Maoni yangu ni kuhusu mali ya asili – mazingira. Katiba ya sasa iliyoko, kitu hutumiwa sasa, kimewapa nguvu sana watu wa mazingira, wizara ya mazingira na wizara ya mali ya asili. Kwa sababu hivi sasa, kuweza kuzungumza, mazingira tulipata kwa namna kadha hakuna ruhusa kukuwa, ikawa ni sheria. Hakuna ruhusa kukata mti, ikawa ni sheria. Pasi napenda sheria kama hii Katiba imerekebishe hapo kidogo, kwa sababu uvuvi ni mti wa mgongo wa mwananchi wa huku kwetu. Miti ndio majamvi yetu, majumba yetu, kila kitu kinategemea hiyo. Lakini sasa iwapo itakuwa sheria, ipite mara moja kwa moja kwa wizara tu kama hivi sasa. Hivi sasa wajua mti fulani hakuna ruhusa ya kuikata. Hivi sasa kama mwambiwa, “Mwangati” hakuna ruhusa mkate. Watu wakifika baraka wanataka kukata mwangati, wakiwa game wanawarudisha rudini hamna ruhusa ya kuukata. Nayo ndio riziki ya kwetu na hatuwezi kwenda anywhere and continue. Kwa hivyo Katiba iweze kuangatia hivyo, badala ya kumlemea mwananchi. Napenda Katiba hapo irudishiwe mwananchi wa kawaida awe ndiye atatoa maoni hapo, washaurianevipi tutarudisha mazingira, sisi tutaendelea vipi?

Kwa upande wa mazingira na mali ya asili – Utaona mali ya asili kama mnyama anahifadhiwa sana. Lakini mahali ikiliwa na mnyama , hahifadhiwi. Yule mnyama ni wako? Hivi sasa ngombe wako akiharibu shamba utamshtaki wapi, ati ng’ombe ameharibu shamba wewe mwenyewe utalipa. Ndovu akiharibu shamba utapelekwa huku, upelekwe huku, upelekwe huku na malipo yakija hailingani na ucharibifu wake. Wakati mwingine ndovu amemuua mtu badala alipwe si kiasi kile amelipwa. Basi iangaliwe, hukumu hizi zirudie kwa wananchi, wawe wananchi ndio wenye kushauriana katika mambo hayo.

Kuhusu malipo katika serikali za wilaya – serikali za wilaya, councillor na mjumbe wako karibu kuwa sawa. Wote wameteuliwa kwa kura. Lakini nashangaa kuambiwa councillor alipwe na baraza, mjumbe wake analipwa na kamati fulani za Bunge. Napenda pia hawa councillor kama wateuliwa na kura na malipo yao na wa Bunge ni mahali pamoja, kama vile mshahara utoka kwa Bunge, ndio mshahara wao ndio utoke. Kwa sababu aambilapo kwa baraza lile Baraza lenye kumleta mwananchi, akafika huko akatupwa huko hapatikani. Hupatikana wakati wa hawa macouncillor kulipwa na Baraza linapoendelea basi naona hii irudi kwao. Pale wanapolipwa wabunge, basi Baraza vile vile wafanyikazi wake walipwe hapo

hapo.

Kuhusu nani aliye Mbunge – Naona yule aliye kuwa ni mwananchi, apewe ruhusa. Kila mtu ameruhusiwa ni mwananchi, aruhusiwe ashirikiane na sisi kwa muda wa term moja. Nani awe ni mwananchi? Mwananchi awe ni mtu wa kuzaliwa kwa mama na baba - - baba ni Mkenya, mama ni Mkenya. Sheria ingine kama vile kuoa kwa kuolewa, kwa njia nyingine inayopatikana kama hivi iliyoko sasa , pia. Bora awe ni mwananchi. Isiwe, mwananchi, tuseme mzazi huwa wa Kenya, Mjerummani kuzaliwa Kenya anao ruhusu kwenda Bunge? Sio tu ni mzaliwa wa Kenya, mwananchi aliye na kitambulisho cha Kenya kuwa ni mwananchi, aruhusiwe.

La mwisho ni mambo ya ufisadi – serikali imetoe pesa nyingi kuifanya hii Katiba. Lau, kama serikali haitaleta kifungu cha ufisadi katika hii Katiba, nani ataifanyia, ataenda kinyume na hii Katiba iliyoundwa, achukuliwe hatua kali, itakua haina maana. Ni kama sasa Katiba hii, lakini utaona ina mambo mengi yanaenda sawa sawa. Utaona sheria tena ya kutoa vitambulisho kwa Kenya ni sawa kwa watu wote. Sheria iwekwe kwangu mimi, iwekwe kwa mtu wa Bara. Kutoa kodi ni sawa sawa kwa watu wote lakini si ufisadi mwenye pesa apeane pesa zake. Mimi kama mwananchi siwezi kuchukua tu hiyo karatasi na siipati Pasipoti kwa sababu ya ufisadi. Ufisadi uangaliwe sana. Iletwe kifungu kwa atakayefanya ufisadi katika Kenya hii, iwe atachukuliwa hatua kali sana. Asalaam Aleykum.

**Com. Mosonik :** Asante. Asman Abud, Faza leaders.

**Asman Abud :** Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu. Niko hapa mbele yenu kuakilisha memorandum ya viongozi wa Faza Location.

Nikianza – Kanuni za kuongoza serikali za (inaudible). Tunaitaji kauli kwenye Katiba zinazoonyesha fastafa ya kanuni ya taifa na uongozi. Kila jamii ifwate mila na desturi za kimusingi. Lakini isiwe na madhara yoyote kwa binadamu. Hapa tunaona Katiba lazima isiingilie mila na desturi za kijamii licha ya hayo, desturi zenyewe na mila siziwe ni kinyume cha haki za kibinadamu.

Maadili muhimu yanoyopaswa kuwekwa kwenya Katiba ni: elimu, afya, haki za kibinadamu, haki za kumiliki ardhi, haki za ugawanyaji pesa hasa kwa mikoa na wilaya, usalama, na nafasi za kazi.

Nne, lazima maadili yatekelezwe kisheria.

Ukuu wa Katiba: tunajua serikali ya Kenya kwa muda wa miaka thelathini na tisa, inatumia Katiba ambayo mwananchi hakujua. Kwa hivyo sasa tunataka kuileza Katiba mpya itakapoandikwa, iwe mwananchi anaielewa, na kuifahamu, na kuitumia ipaswavyo.

Bunge – Kubadilisha Katiba ipatikane asili mia sabini na tano (75% ) ya kura zote za Wabunge. Kwa hivyo Katiba iliyopita ilikuwa kubadalisha Katiba ama sheria kupitia Bungeni ni asili mia sitini na tano (65%). Hicho kiwango kilifanya Katiba ya Kenya kubadalishwa mara thelathini na mbili bila mwananchi kushirikishwa. Ilikuwa ni mchezo Wabunge wanacheza na watawala wakiwa Bungeni, Katiba ilibadilishwa bila sisi kufahamu. Kwa hivyo kifungu cha 65% kiondolewe, kimechezewa sana, na Katiba imechezewa sana. Kipelekwe mpaka kifungu cha 75%.

Sehemu ya Katiba inayo husiana na dini, mila, na mambo yanayohusu wabunge, ibadilishwe. Wananchi wahusike kubadilisha Katiba inayoafikiana na dini, desturi na mambo ya wabunge. Kisha, haya mambo ya Katiba ikibadilishwa, isiwe ni kupitia kwa Bunge tu, bali viongozi, wananchi na wakaji wa mahali mbali mbali wawe ni wenye kutiliwa katika mafanikiyo hayo. Mikutano ya maoni iongozwe na Tume. Kama hapa leo tunapofanya.

Uraia – raia wa Kenya bila swali ni mzaliwa wa baba na mama. Huyu hana swali lolote. Sio kama saa hii tunapelekwa juu na chini kuuakilisha uraia wetu wa halisi kwa mtu: kama atoke Kisumu, Nyeri, Nairobi, Nakuru anakuuliza wewe, ukienda ofisini unataka kitambulisho, unataka Passport. Mtu akiwa yeye amezaliwa Kenya kwa baba na mama, huyo ni raia halisi.

Utaratibu mwengine wa kuijandikisha kama uraia ni ule wa waume au wake bila kuzingatia jinsia. Usiwe uraia utapewa mume tu, mke asipewa, hiyo isiweko katika Katiba. Mtoto aliyezaliwa na mzazi mmoja ambaye ni raia wa Kenya bila kujali jinsia ya mzazi huyo, apewe uraia. Hii nafikiri imetangulia kusemwa. Raia awe na haki zote za kikatiba. Haki na majukumu ha raia yategemea uraia namna unavyopatikana. Raia halisi awe ndio atakuwa na majukumu zaidi kushinda yule raia ambaye ataandikishwa, ama atapata katika njia nyingine. Katiba iruhusu raia wa nchi, isiruhusu raia wa nchi mbili. Kama haya mambo yanapatikana baadhi ya nchi, hata kama nthini Kenya.

Wakenya wawe na cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha kitaifa. Kwa sasa watoto wenye wamezaliwa juzi juzi, kitambulisho kinasema wazi ya kuwa - - si thibitisho ya kuwa raia wa Kenya. Hii Katiba inataka iondoe mara moja. Unapozaliwa, uwe ukipata kitambulisho, uwe ni mwenya kupata uraia bila uswali.

Ulinzi na usalama wa taifa – vyombo vyaya usalama, majeshi na matawi yake yaundwe na Katiba, sio kupitia kwa nguvu za Rais, ama kwa nguvu za serikali. Kunidhamisha majeshi na silaha yapelekwe katika mahakama ya kiraia. Hivi nasema mfano: mwanajeshi anapofanya kosa la kiraia, ni lazima apelekwe katika mahakama ya kiraia. Ni juzi tu mwanajeshi mmoja alishikwa na dawa za kulevia, na wanajeshi wenzake wakamfwata akiwa polisi Lamu, na nilikuwa hapo.

Rais awe amiri jeshi mkuu wa majeshi ya silaha. Mamlaka ya nchi yawe na uwezo kamili wa kutangaza vita, kama yakiwa yawe ni yenye kutokea. Katiba iruhusu uwezo wa kipekee katika hali za hatari kama vile vita, majanga ya kitaifa, maasi ya kukosekana kabisa kwa usalama wa umma. Mtawala wa sehemu inayohusika na hatari, awe na uwezo wa kutangaza vita au

majanga fulani. Hii utaona panapotokea dharura mpaka mtu aulize order kutoka Nairobi. Hili nishalionia Kiumba, Morgan alipoingia polisi na wanajeshi meli waliokuwa Kiunga, walishindwa watafanya nini. Ikabidi kila mtu aende atafute pale atapoingia. Ikipigwa simu patroli ama radio call, wanasema tunangojea order kutoka Nairobi. Pale pale ilikuwa ni DO, awe na uwezo wa kuambia askari watangaze vita mara moja.

Bunge liwe na jukumu lolote la uwezo huu wa hali ya hatari. Kwa hivyo hata Wabunge wawe wenye kupelekwa kukitokea hali ya hatari.

Vyama nya kisiasa – vyama vy kisiasa vitekeleze majukumu mengine licha ya kuwahamasisha wananchi, kama mfano ujenzi wa kitaifa. Sio vyama nya kisiasa viwe vitakwenda kwa upande wa siasa tu, na kujenga ukabila kama vile tunavyoona. Katiba ieletez uwandaji, uongozi, na tabia za vyama nya kisiasa. Katiba iwe: kama chama ambacho kitakuwa kina sifa ya ukabila, basi kipigwe marufuku mara moja na Katiba. Kuwe na jumla ya vyama viwili tu nya kisiasa, kwa sababu ya kupunguza ukabila, na utumishi wa pesa za serikali, pasipokuwa na usawa. Kila chama kijigaramie chenyewe. Vyama nya kisiasa visigaramiwe na pesa za umma. Kwa hivyo mtu anapo unda chama, ajuwe wapi atatoa pesa za kupeleka hicho chama chake. Dola za vyama nya kisiasa wasishirikishwe katika kujenga taifa. Kwa hivyo dola na vyama nya kisiasa kama, tuseme wakati kama huu, ambao tunaona chama cha KANU kikiamua ni dola iwe ni kwa watu wote, kikiamua ni siasa iwe ni upande wa KANU. Lakini tusichukue mali ya umma, kama kuna mali ya umma mengi imehadhibishiwa chama cha kutawala, bali si mali ya asili.

**Com. Mosonik:** Time imekwisha.

Miundo ya aina ya serikali – tufwate muundo wa serikali ya majimbo. Kazi za serikali zitakuwa rahisi tukifwata muundo huo. Kupunguzwa ufisadi na pesa za umma:

**Com. Mosonik:** Kama umesema majimbo imetosha, what is the next point?

**Asman Abud :** Kwa ufupi hapa – Bunge: Bunge lipige msasa wa darubini uteuzi wa maafisa kama, Tume, Makatiba wakuu, wakuu wa mabenki ya serikali, mahakimu na Makadhi, wakuu wa mikoa, mabalozi. Kwa hivyo Bunge lisiachie Rais kufanya kazi hii ama serikali. Majukumu ya Bunge yapanuliwe kwa kuchagua maafisa waliotajwa katika nambari ya kwanza. Bunge lisiwe na uwezo usio kikomo wa kuthibiti taratibu zake. Kazi za ubunge ziwe ni za kila siku. Kusiwe na mabadiliko yoyote kwa wapigania kiti cha Urais, bali mpangilio: kiti cha ubunge awe na miaka kuanzia ishirini na tano kuendelea. Kwani ilikuwa ni miaki ishirini na moja, hapa sasa tunataka iongezwe iwe ishirini na tano, kupigania kiti cha ubunge.

Mitihani ya lugha ya kitaifa ichunguzwe na wabunge- - - (inaudible interjection).

Mada ingine ilikuwa ni mamlaka ya nchi. Katiba ifafanua masharti ya kutimizwa kwa ugombeaji kiti cha urais. Mgombeaji awe

na umri wa miaka 35 mpaka miaka 60, sio mtu akalie kiti tu. Awe ni mzaliwa wa Kenya wa kuzaliwa. Awe na elimu ya kutosha kiwango cha degree. Awe na afya nzuri asiwe na kilemu. Mtu mwenye sifa nzuri asiwe na makosa ya aina yoyote. Awe amekuwa Mbunge kwa vipindi visivyo pungua miaka miwili. Awe na kiwango kikubwa cha pesa zinazojulikana. Sio Rais awe maskini. Awe na kiwango cha pesa ambacho kupitia kwa statement za bank, atathibitiwa na zitatangazwa. Rais awe na kiwango maalum cha uongozi. Awe kwa kipindi kimoja cha miaka mitano. Baada ya kipindi Rais abadilishwe kwa majimbo tofauti, tofauti.

**Com. Mosonik :** Asante. Peleka memorandum upande ule mwengine, please. Asante kwa memorandum hiyo, tumsikize, please Zakaria Omar – Muslim Imams – Faza.

**Zakaria Omar :** Salaam Aleykum wa rahamtulilahi wa barakatu. Mimi nitatoa maoni ambayo pia yametolewa kwa wingi lakini kidogo pengine nitakuwa na mazidisho.

Ningependa kuanza na Kadhi – Nasema Kadhi achaguliwe na Waislamu, Mashehe na maimam. Lazima awe na elimu yakatosha: amesomea sheria ya Kislamu kutoka Chuo kikuu cha Kislamu kinachotambulika. Mahakama ya Kadhi igawanyike sehemu mbili: yaani igawanyike mahakama ndogo, Kadhi's subordinate na vile vile igawanyike sehemu ya pili ikiwa ni High Court, mahakama kuu ya Kadhi. Iwekwe kamati maalum ya masheikh ya kuwafanya mtihani wa ukadhi wanaotaka Kadhi achukue ukadhi.

Lazima achunguzwe: miendo yake, tabia yake ni nzuri, hakushikwa na makosa makubwa, makosa ya jinai, vile vile awe ameo. Kuna makadhi wengine watafuta wanawake ----kwa hivyo inalazimika awe ameo. Umri usipungue miaka thelathini. Awe anajilazimisha na mambo ya ibada, si kwamba ajilazishe lakini hatumuoni kama anasubiri kwenye ibada. Awe ni (inaudible) vile vile awe anajishugulisha na mambo ya Uislamu. Awe akijishugulisha na maendeleo ya Kislamu. Ahukumu kwa kitabu (inaudible) wa suna torati kumi, kitabu cha Mwenyezi Mungu ni Quran na sura ya Mtume inajulikana, kwamba ni hadithi sahihi ya Bwana Mtume (P.B.U.H).

Pia iweko Kadhi Court of appeal. Huu uwe ndio mwisho wa court na isirudiwe tena kupelekwa mahali pengine popote. Chief Kadhi lazima awe anakitumikia ukadhi kwa muda usiopungua miaka kadhaa. Kwanza awe Kadhi akishafanya miaka kadhaa, kisha achaguliwe kuwa Chief Kadhi, kwa sababu awe na uzoezi wa hii kazi ya Chief Kadhi. Au awe ametumika kwenye maktaba ya kadhi. Kadhi na Chief Kadhi wahusike na kutoa hukumu tu peke yake, na kutoa repoti. Mambo mengine yasimamiwe na kiongozi aliyechaguliwa na Waislamu. Wasaidizi wa Kadhi, wanaosadiki ndoa na kadhalka. walipwe mshahara.

Hukumu ya ndoa na talaka zihuusike kwa Kadhi, badala ya kwenda kwa hukumu ya kanuni yake.

Cheti za watoto wenyewe kutupwa na mababa zao, kislamu ziende kwa Kadhi badala ya kwenda kwa office ya watoto.

Pia Makadhi waongezwe ili hudumma iwe karibu zaidi na wananchi waIslamu.

Cheo cha Chief Kadhi kiwe ni kama cha Judge, Judge mkuu wa Kenya (Chief Justice). Pia mshahara uwe sawa sawa - - anaopata hu Judge na anaopata Chief Kadhi.

Sasa nitaingia upande wa elimu. Waalimu wa dini walipwe mashulen na wale wanaosomesha madarasa pia walipwe sababu wanafanya kazi moja. Kwani ushuru unaopatikana na malipo kwa serikali kama mapato yake wahusu wananchi wote. Wakati uwe sawa kwa masomo ya dini na ya shule.

Vazi la Kislamu liwe lazima: hijab kwa wasichana na wanaume vaazi linalokubaliwa na Uislamu.

Wasichana na wavulana wasichangamanishwe kwenye mashule, wakae mbali mbali.

Kuhusu mambo ya siku kuu. Siku kuu, siku ya Ijumaa, iwe siku kuu kama siku ya Jummapili wala tusishugulike. Ille imefanywa na ikaingizwa kwenye serikali ili kupatia utukufu ukristu na kama kweli. Na tunataka iiingizwe, kwa Kislamu, Ijumaa. Pia siku ya Arafa iwe siku kuu kama siku ya Idd-Ul-Fitr: ni kwamba tutafunga siku hiyo na ni siku ambayo ni tukufokusana ya ushindi, kwa hivyo lazima iheshimiwe.

Matangazo ya dini: Waislamu wawe na matangazo ya dini kwenye idhaa sawa sawa na matangazo ya Kikristo. Ikiwa hawa kwa wingi madharani wana vipindi kumi na moja, na Waislamu vile vile wawe na vipindi kumi na moja.

Matibabu – Hospitali kuwe na madakitari wa kike wanaohudumia wanawake, na wakiume wanahudumia waume. Hii ndio kislamu tunaotaka, kufanya kinyume ni kuiingilia Uislamu.

Usawa wa haki: Mwanaume apewe haki kulingana na jinsia yake, sio haki sawa. Na mwanamke kulingana na jinsia yake, wala sio kupatikana msemo - - inataja kuwa mwanaume na mwanamke ni sawa sawaa: Katiba iwache lazima tuwe na tofauti. Kwa sababu Mwenyezi Mungu mwenyewe alileta tofauti.

Mali ya Waislamu – Mali ya Waislamu wakufu irudishiwe Waislamu wenyewe na tahasisi zilizochukuliwa na serikali zirudishwe kwa Waislamu. Kama Chuo kikuu Therani na (inaudible) --- haya ni mali ya Waislamu. Na nyengine yote yawe mikononi mwa Waislamu iliyochukuliwa na serikali. Mambo ya ibada: Ibada ya Hijja mtumishi wa serikali apewe mwezi miwili kujitayarisha, sababu ana safari yake. Naulizwa kabisa maoni yoyote yatakayokwenda kinyume na sheria ya Kislamu, yasizingatiwe, yatupiliwe mbali, na ipigwe teke. Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu.

**Zakaria Omar Sidiqi :** Jina langu ni Zakaria Omar Sidiqi na nimeakilisha Ma-Imam, na waalimu wa dini ya Kislamu hapa Faza – shukrani.

**Com. Ahmed Hassan:** Sasa nafikiri tumekaribia wakati wa adhuhuri, na ninafikiri ni wakati mzuri ambapo tungeairisha hiki kikao ndio turudi saa nane na nusu. Tuende lunch halafu tutarudi saa nane na nusu. Salaam Aleykum wa Rahmatullahi Wabarakatu.

**Break for lunch:**

**After lunch:**

Ya tatu : Katiba - Tuifwate vile vile kunitiradhi kwa Kislamu, vile itafuata ilivyosema Quran. Mwanaume mafungu mawili na mwanamke fungu moja kutokamana na Quran.

Ya nne – Basingiti wa Makadhi walipwe mishahara kama wengine katika nchi hii.

Jambo la tano – Katiba ikubali sisi Waislamu tuweze kuhukumiwa na kitabu cha Mwenyezi Mungu.

La sita – Na hili ndilo la mwisho. Masheikh wa Kislamu au wanachuoni wa Islamu wachaguliwe, wawe wenye kutambuli na serikali katika mambo ya Kislamu. Ili litokeapo jambo la Islamu watangaziwe zaidi Sheikh wa kislamu au wanachuoni kutengeza mambo yale kuliko watu wengine. Kwa haya, Salaam Aleykum....

**Com. Mosonik :** Asante. Sasa tutasilikiliza Ali Bunu kwa niaba ya wakulima.

**Ali Bunu :** Salaam Aleykum. Jina langu mimi naitwa Bunu, na nimefurahishwa kuona jambo hili la Katiba. Ikiwa itakuwa kweli, Katiba, basi naomba Mungu aulinde mkataba huu.

Kitu cha kwanza nitakacho mimi katika, kwa niaba ya wakulima, Katiba hii iundwe na isajiliwe kwamba serikali iwe ya Majimbo. Sasa serikali ikiwa ya majimbo, na lile jimbo litakuwa la Kislamu basi hukumu ziwe ni za kislamu. Kama Kadhi Mkuu awe pia mkuu wa sheria kama Attorney General, ye ye atatuhukumu kislamu. Awe na ofisi yake na wale ambao wenye kuhukumu wawe yake.

Kitu kingine – Kuhusu upande wa Mali ya Asili – kama ardhi, bahari, kila kitu. Serikali naiomba sana isiingilie katika mambo

ya bahari, iwachie wenyewe wananchi wajiamulie vile namna wale walioko watajua namna ile ardhi itumiwe. Sio serikali ichukuwe watu kutoka nje, wazungu, waletwe wawe wasimamizi wetu. Hili shirika---(tape blank)

Msitu na bahari - hicho kitu kabisa – baada ya muda lazima kutatokea mambo mabaya sana. Na Katiba hii itakuwa Katiba mbaya sana.

Na kitu kingine nataka kuzungumzia ni kwamba kuhusu kwa kuchaguliwa kwa Ma-Imam. Na kwamba Kadhi achaguliwe na wale wanachuoni ambao wamesoma, wenye elimu ya juu kabisa. Tena achaguliwe kwamba ni mtu ambaye alisoma dini, akiwa yuko sawa, mpaka akaenda katika vyuo vikuu ambao amesoma dini. Sio mtu awe hajasoma skuli, akisoma elimu na Kizungu hawezি kuchaguliwa kuwa Kadhi Mkuu. Hicho kitu kabisa kisiweko.

Na kitu kingine ni kuhusu Bunge – Wabunge walioko katika Bunge - - kwa sababu hi Kenya watu wengi wanaelewa lugha ya Kiswahili - - sio wabunge wawe wanazungumza kizungu kama wale wazungu. Wazungu wako kwao Uzungu. Hapa tuzungumze Kiswahili ndio lugha ya hii taifa. Lakini sio kwamba lugha ya taifa utupwe tuige Kizungu, wao wasiongee Kizungu kabisa, Katiba hii mpya ikataze kabisa.

Na kitu kingine ni kwamba hawa wabunge wakichaguliwa, pale pale wamechaguliwe, wajenge makao pale wakae pale. Wakimaliza sehemu za bunge waende nyumbani. Bibi zao na watoto wao wakae zile sehemu, ikitokea shida yejote waweza kupata habari. Sio mtoto wa mbunge, halafu yeye aende Nairobi huko, halafu mambo ya huku nyuma hajui dhahiri kumetokea nini wala kuna shida gani.

Kiko kitu kingine cha Katiba: labda serikali atatuhurumia namna hii, litakuwa ni jambo hatari sana hata sehemu hii, ikiwa serikali ataleta mshirika ---na mpaka saa hili linaendelea. Kuna shirika zimeletwa hapa za Mzungu, hata kumwomba Mungu wasikia kazi (safari ndani yaho tume--- shirika hili ku---tupate masilahi safi nao unakuta masila (inaudible)

Kwa hayo sina mengi. Salaam aleykum.) heavy dialect influence.

**Com. Mosonik :** Asante. Sheikh, Councillor Omar K.

**Councillor Omar Kassim :** Mimi ni Councillor Omar Kassim -

Kwanza ningetaka kutilia mkazo neno hili la citizenship. Ningependa kwamba tatizo la citizenship: liwe ni mzaliwa wa sehemu hiyo ndio anaweza kupata kila kitu sawa na mzaliwa. Na asikuwe tofauti na mzaliwa mwngine ambaye pengine ameomba uraia huku. Kwa mfano katika haki za umilikaji wa ardhi, katika haki za kisiasa (inaudible).

Jambo lingine ningependa kuzungumza ni kuhusu foreign affairs. Ningependa Kenya iweze kutambua marafiki wale wa kushirikiana nao. Kwa mfano kama taifa la Israel linavunja haki za Uislamu vile vile linavunja haki za Ukristo. Kwa hivyo

ningeona kwamba itangazwe pia kwamba Israel ni katika taifa moja la terrorism, lweze pia kutengwa na tusiwe na uhusiano wa kibalozi na Israel.

Land – Tatizo la ardhi nimeona kwamba ni tatizo sugu ambalo limewasumbua Wakenya wengi. Kwanza tumeomba kwamba sheria za Trust land ziundwe kila community ambao ni wenyewe wanaishi kwa hizo ardhi, iwe ni trust land wao wapewe, umiliki kwa hiyo ardhi. Tuseme ardhi ambayo imezungukwa na bond trust land, kama ardhi ambayo imekaliwa na Bajuni kwa miaka elfu mbili, iwe ni Bajuni trust land, isiwe ardhi ya kila mtu. Watu watoke Murang'a, Kiambu, Kano, Western waseme ardhi hii ni ya watu wote. Maana tunasema hatuwezi hili, tunabaguliwa, na hatuwezi kupewa ardhi za kukaa katika sehemu zingine.

Government Structure (Yaani utaratibu wa kiserikili): Tungeomba serikali hii iwe na Rais ambaye uwezo wake umekuwa ukipunguzwa. Awe chini ya sheria, sio kuwa juu ya sheria. Kwa sababu akiwa Rais ni juu ya sheria, basi mambo yote atajiwekea: vile atachagua Ma-PS, Judiciary --- na kadhalika. Tuseme tuwe na Prime Minister ambaye atashugulika na mambo ya executive. Vile vile tuwe na Deputy Prime Minister wawili na Vice President wawili, kutoka ile winning party. Kuwe na vyama visivyozidi vitatu, katika serikali. Vyama vingine vitupiliwe mbali ambavyo havitakuwa na msingi thabiti ama vina msingi wa kikabila.

Jambo lingine ningependa kuzungumza ni kuhusu Electoral Commission – Electoral Commision iwe inachaguliwa na Bunge: Iwe watu wanaomba, majina yao yapelekwe katika Bunge, halafu Bunge ipitishe, iseme hawa ndio watakuwa ni Makamishna. Sio awe President ana uwezo wa kuchagua Tume ambalo anataka yeye. Tume na haki lisiwe likichaguliwa na Rais. Tunaona kwamba Tume la uchaguzi ndiyo itakuwa na uwazi. Sio kwamba niko kazini baada ya siku tatu ama miezi miwili mara nafutwa. Taratibu kama hizi tunaomba zitupiliwe mbali.

Local Government: Local government ni ile serikali ya wilaya na mitaa. Ningemba kwamba Councillor achaguliwe angalau amehitim, isiwe amepungua kilasi cha saba, ndio mambo mengi atawezu kuyafahamu, sio tu kusoma na kuandika. Kuliko kuchagua watu ambao hata kwa hakuona.

Ningeomba vile vile, powers of government officers ziwe reduced. Kama Clerk of Council, uwezo wake upunguzwe. Clerk aweze kuchaguliwa na committee ya Council. Asiwe atakuwa answerable to the Permanent secretary. Council ipewe uwezo wa kuandika na kufuta, isiwe ceremonial. Awe councillor au Mayor, atachaguliwa directly na wananchi. Kuweko na good conduct. Mtu kuchunguzwa tabia yake. Vile vile councillor achaguliwa akiwa na mali. Kiasi siyo millionaire, angalau awe kiwango cha chini ,awe naelfu hamsini. (inaudible). Councillor anaweza kuchaguliwa kulingana na wisdom of leadership. Awe na historia ya uongozi: tangu zamani ashawahi pengine kuongoza hata--- lakini siyo mtu kuchaguliwa hana rekodi yoyote ya uongozi.(inaudible).

Natural Resources - Mipango yoyote itakayo fanywa kuhusu natural resources, lazima wanakijiji washirikishwe. Siyo

itachukua mtu Research kutoka kwa university ya Nairobi waseme jambo ambalo halikuambata na hali ya mazingira ya hapa. Tungeomba kwamba research yoyote itakayoguza natural resources, kwa mfano kama mikopo, misitu, maji na kadhalika, iwe Wanakijji wanaweza kushirikishwa.

Jambo lingine ni Police – polisi wawe watafundishwa mafunzo ya maana, ili waweze ku-handle wananchi. Kwa mfano kama polisi wa Tanzania, wanafundishwa taratibu mzuri za kushika wahalifu, siyo taratibu kama hizi za Kenya ambazo hazina uaminifu na nchi. Ningombwa kwamba polisi wasiwe station zaidi ya masaa sita. Na kama wanataka kufanya search, wahakikishe kwamba search yenyewe inafanywa kwa njia ya haki. Mtu akipatikana na makosa, aweze kujicukulia bond yeye mwenyewe. Si lazima awe na title deed ama pesa. Yeye mwenyewe anaweza kujisimamia bond hiyo. Kama vile taratibu ya waTanzania hufanya. Polisi kama hao vile vile wawe wamesoma zaidi ya Form four.

Viongozi wa serikali: tunaomba serikali iondoe vyeo kama DC, PC, na DO. (Vyeo kama hivi hatujaona umuhimu wake, serikali inaharibu pesa.) Kwa mfano utakuta kwamba hii ndio kama elective power katika office ya district. Anafanya vile ananyotaka, utakuta kwamba kila kitu kitakuwa chini yake. Hata akiiba hakuna utaratibu wote unaweza kumfwata kwa sababu yeye ndiye mambo yote. Yeye ndiye security board chairman, land control chairman. Kwa hivyo uwezo huo apewe Chairman to the council au Mayor.

Uwezo wa Machief upunguzwe, kama uwezo wa pengine kuchagua ma-headmen kuwe umepunguzwa. Chief pia awe na tabia nzuri (of) good conduct, achunguze tabia yake. Awe na elimu ya Form four, awe na C+. Asichaguliwe kwa njia ya mlango wa nyumma, au kwa njia za kisiasa zingine. Awe angalau amepata administration. Ama achaguliwe kwa njia ya mlolongo, ikiwa atapitia administration.

Accident ---- Taratibu za barabara lazima zichunguzwa ziwe na sheria zake. Utakuta kwamba mtu anapeleka gari hajali. Kwa hivyo taratibu hizo lazima zichunguzwe na mtu kama akisababisha ajali katika sheria za Kenya afungwa, alale cell, apokonywe hati ya kuendesha gari. (inaudible) Kama hizi taratibu za barabara vile vile wanapofanya zile hati zao hawashirikishi ile community.

Game Reserves – Reserves hizi tunaona ziondolewe. Kwa sababu badala ya community wafaidike, hakuna cheti chochote hupatikana kwa game reserve, badala yake yameleta mateso makubwa kwa wananchi amba hawana vyeti. Na usimamizi wao mara nyingi umekuwa wakisimamiwa na serikali. Angalau kama ulikuwa usimamizi wao unasimamiwa na Game Ranger ambaye ni local – wa hapo ingekuwa afadhali. Kwa hayo machache, asanteni.

**Com. Mosonik :** Abud Omar, Abud Omar yuko? Okay Abud Hamid

**Abud Hamid :** Kwa jina naitwa Abud Hamid, kutoka Pate Location. Hapa mimi kwa niaba ya watu wa Pate Location nina

memorandum. Nitasoma mapendekezo kurekebisha Katiba ya Kenya.

Nitaanza na sehemu ya Uraia – Number one : atakayekuwa raia wa Kenya bila swali ni yule ambaye amezaliwa Kenya kwa baba na mama. Two: utoaji wa uraia wa Kenya ufwate taratibu ile ile ya kawaida, yaani kwa kuzaliwa, kwa kuandikishwa na kwa jinsia. Waume na wake wawe raia wa Kenya, bila ya kuzingatia jinsia wapewe uraia wa kuandikishwa. Mtoto aliyezaliwa na mzazi mmoja ambaye ni raia wa Kenya, bila ya kujali jinsia ya mzazi huyo, apewe uraia bila kwazo. Raia ana haki zote za kimsingi: kama kuishi salama, na haki ya----na ana jukumu la kulinda na kutetea nchi yake. Katiba isiruhusu raia wa nchi mbili direct. Wakenya wawe na vitambulisho vile vile vya kawaida iliyoko sasa.

Kitu kingine kilikwa ni kuhusu muundo na aina ya serikali – Wananchi wa Pate location waliamini wakajadili kuhusu aina ya serikali ambayo iliyoko. Na kwa zaidi wao wanapendelelea kufwata muundo wa serikali ya Majimbo: ambapo mamlaka ya nchi hii na Bunge, yatagawanywa baina ya serikali kuu na serikali ya Majimbo, tukiwa na kura kubwa ya serikali. Tatakuwa na Bunge yetu kujimulia mambo wenyewe, kulingana na jimbo letu. Two, tunaendeleza uchumi wetu. Three, nafasi za kazi kwa watu wetu zitapatikana. Hatimaye kwa wazee wangu, tulitependelea pia baina ya serikali na majimbo, ama sivyo?

**From the floor :** Ndio.

**Abud Hamid :** Sawa sawa. Kwa hivyo Bwana Commissioner ningependa kuemdelea na swali la pili, wananchi wote wanapendelea serikali ya majimbo.

Sehemu ingine ni kuhusu mahakama – Uhuru wa mahakama uliyoko kwenye Katiba ya sasa, kiwango cha juu cha mahakama ni mahakama ya rufani. Tukifika hapa, hatuhitaji mahakama kukaa zaidi ya hiyo. Two, maafisi wa mahakama wateuliwe na kamati zitakazoundwa na Bunge katika serikali kuu. Three, Kadhi mkuu na Makadhi wateuliwe na baraza la Ma-Imam, kwa njia ya kutahiniwa kwa sakafu. Wakishapita mtihani, baraza la Ma-imam litapendekeza majina yao kwa serikali, kuwa ndio ma-Kadhi wameteuliwa. Kwa sababu ya kazi Kadhi lazima watumize masharti yafwatayo: Kadhi Mkuu – lazima awe anadumu na makadhi kwa kipindi kisichopungua miaka kumi, awe mwaadilifu katika kazi, na elimu ya kutosha. Makadhi: lazima wawe na elimu ya kiwango cha kidato cha nne angalau, wawe na cheti, wawe na elimu ya dini ya kutosha - - haswa kwa upande wa kurhani na kadhalika kuhusu mambo ya dini - - wawe na tabia nzuri na uadilifu.

Fungi No.5, Kuhusu Mahakama: Mahakama ya Kadhi ishugulikie makwaza ya ndoa, talaka na urathi, na haki za watoto. Wawe ambaao wa kike, wakawa Waislam, hawa watoto wakiwa wadogo, ama wafanya talaka na wanawaacha watoto wadogo katika hila za mama zao. Kwa hivyo pendelezo katika marekebisco ya Katiba ya watu wa Pwani, tungependelea kwamba hii nafasi m iongezewe makadhi iwe ni jukumu lao waweze kuhudumia, sio kwamba yapelekwa kwa maafisa wa watoto.

Kitu kingene ni kuhusu serikali za mitaa:

Number one, mayor na mwenyekiti wa Baraza wachaguliwe moja kwa moja na wananchi.

Two, vipindi vya miaka miwili kwa mayor na wenyeviti kwa baraza vyatosha.

Three, mabaraza yaendelee kufanya kazi chini ya serikali kuu, ambapo hapa, kama tulivyosema kabla, kwamba wananchi wanapendelea serikali ya majimbo. Uwezo ugawanyiwe upewane vile vile kama kamati.

Four, eneo ya chini zaidi kwa madiwani: lazima mtu awe amesoma mpaka kidato cha nne na amepata cheti, bila kuwa na cheti mtu atakuwa kidato cha nne pengine ameanguka, au kwa bahati mbaya hakufanya mtihani. Kwa hivyo atakuwa ye ye atakuwa ni mbali kuwa diwani.

Basi wa mitihani ya lugha inayofanywa na wagombea viti vya udiwani inatosha.

Kuwe na masharti ya maadili na tabia kwa wagombea viti vya udiwani: ndio mtu asiwe hadharani tu akiwa anataka kugombea kiti cha udiwani lazima awe ana maadili fulani ya kitabia, na wananchi ndio watosheke nayeye.

Seven, Wananchi wawe na haki ya kumregesha nyumbani diwani, kupitia kura ya kutokuwa na imani naye, ikiwa atakuwa hana uadilifu katika kazi zake.

Eight, atakayefanya kauli kuhusu mshahara wa ubunge na wa udiwani iwe ni serikali kuu,

Nine, Bunge lenyewe liwe na uwezo wa kuvunja mabaraza.

Kuhusu mazingira na mali ya asili – Wananchi wa Pate Location walipendelea kwamba kuwe na usawa kwa manufaa katika mali ya asili. Na 50% la pato litumike kuendeleza mazingira hayo. Ujira uwe kwa wakaazi wa masingira hayo, hayo, kwanza, kisha kama kuna ziada ndio mtu mwengine afikiriwe.

Kitu kingine kilikuwa juu ya Ardhi na Maji – Serikali izuie udhaifu na umasikini wa raia wake. Stakabathi za kumiliki ardhi ziondolewe nchini, hata kwa wilaya. Two, wananchi wewe huru kununuua, kuuza na kumiliki ardhi kwa matumishi halali popote nchini.

Kitu kingine kilijadiliwa na wananchi wa Pate location ni kuhusu uongozi kwa matumizhi ya mali ya asili.

Mashirika ya serikali ambayo yaundwa na watu binafsi ikiwa ni kuundwa, pia wakaazi wapewe nafasi ya kwanza, wa eneo hilo, lenye mali ya asili

Maafisa wote wanaoenda kinyume na maadili ya ufanyaji kazi na matumishi ya pesa, mali ya umma, na huduma za umma, katika jamii washtakiwe.(inaudible) Fedha au mali yaliyopotezwa yarudishwe.

Tume ya maendeleo ya kitaifa – ifikirie kusambaza huduma za maendeleo kila wilaya na sehemu za kuakilishi Bungeni.

Na kitu kingine kile kiliungwa na watu wa Pate Location, ni muundo wa utaratibu wa uchaguzi: katika uchaguzi mwenye kura nydingi zaidi sanandiye mshindi lakini awe amepita kwa asili mia hamsini (50%). Iwapo kiwango hakikufikiwa kwa asili mia hamsini (50%), uwe na duru la pili kwa mshindi wa kwanza na wapili.

Three, Walemvu na akina mama wawe na viti maalumu katika uwakilishi Bungeni.

Katika kugusa uchumi wa nchi na maendeleo katika nchi:

Kuguza kwingine kulikuwa ni kuhusu haki za kimsingi: Serikali iwe na jukumu la kuhakikisha, na kuudumisha haki za kimsingi zote. Two, elimu iwe ya bure hasa elimu ya msingi kutoka darasa la kwanza mpaka la nane. Three, uhai wa raia ulindwe na ku heshimawa . Four, huduma za majadiliano katika Bunge: Inapoendelea iwasilishwe kwa wananchi moja kwa moja kupita Radio kama vile Tanzania wanafanya.

Tuseme, mwisho ni kuhusu Bunge: Ili Katiba ya Kenya iweze kufanyiwa mabadiliko ni lazima iungwe mkono na asili mia themanini ya wabunge, badala ya asili mia sitini na tano. Ikiwa maoni ya watu wengi yatachukuliwa kurekebisha Katiba,kisha igeuzwe na wabunge wapatao asili mia sitini na tano, idadi hii itakuwa ni ndogo sana. Two, umri wa kugombea kiti cha Bunge uwe ni kuanzia miaka ishirini na tano badala ya miaka ishirini na moja. Maana ukaona kutoka miaka kumi na nane mtu huwa na akili ya kitoto, lakini akiwa na miaka ishirini na mitano akili wenda kuanza kukomaa. Three, wananchi wawe na nafasi ya kumregesha nyumbani, mbunge wao kwa kupigia kura ya kutokuwa na imani naye. Ikiwa mbuge hategemezi wajibu wake kwa watu waliomchagua,kura ya kutokuwa na imani iwe baada ya miaka miwili. Baada ya kwenda bunge itakuwa na hatekelezi wajibu wake anapotea potea,haonekani, kama yule mwenzangu alivyosema, huwa mtu anachaguliwa kisha anaenda kuishi kama Nairobi au Mombasa na wale wananchi walimchagua hawamuoni na wana taabu, mtu kama huyo baada ya miaka miwili apigiwe kura ya kutokua na imani. Shukrani.

**Com. Mosonik:** Kuna ahmed A. Sholo, wewe ndio Sholo?

**Sholo:** Ehe—

**Ahmed Sholo :** Salaam Aleykum..Jina langu naitwa Ahmed Sholo (inaudible). Kwamba mambo mengi yamesemwa, na sitaki kurudia yale yamesemwa. Nitaongeza kitu ambacho hamjasema mbeleni. Hii Katiba hii mpya ningependelea kwamba, kuwe na automatic promotion after every five years, yaani upgrading kwa civil servants and teachers who have worked for seven or five years.

Utapandishwa cheo utoke grade ile ulianzia kazi uende grade nyingine.

Pili kuna special teachers na nursery school teachers ambao wanalipwa mshara kwa taabu.Kuwa na tume maalum ya kuwalipa sio council kama ilivyo sasa.

Na kitu kingine ambacho nitawazungumzia ni kuhusu biashara. Kuna hawa wafanyi kazi za biashara kama: hawkers, tailors, bakery shops na hawa kila mwaka wanatozwa ushuru, na County council au Minicipal council au City council. Kwa hivyo Katiba hii mpya tunasema iondoe taratibu hiyo. Hawa watu wanao biashara ndogo ndogo kama hawkers wafanye biashara bila malipo yoyote.

Jambo lingine ni kwa upande wa elimu: tunapendekeza elimu ya msingi iwe bure lakini tunaona afadhali zamani kuliko sasa. Wazazi wanahangika zaidi sasa kuliko zamani, kwa sababu zamani kilikuwa ukilipa fees - - kama sisi tulisoma na 25/= per term hatutoi kitu chochote, yaani books na vingine, ilikuwa ni serikali au shirika kidogo likilipa. Lakini sasa ngumu, kuna kitu kinaitwa cost sharing. Yaani mzazi anashugulika kununua au analazimika kununua kila kitu ambacho kinahitajika kwa mwanafunzi, kama vitabu na vitu vingine. Kwa hivyo tunaomba Katiba hii mambo ya cost sharing yaondoke. Katiba mpya italazimisha serikali itoe vafaa vyovyyote ambavyo vyatakitana kwa watoto kusomea kama vile vitabu.

Na mwisho tunasema kwamba – Mali na hati ya kimiliki iende kwa mzaliwa kwa baba na mama. Ikiwa ni mzaliwa kwa kujuandikisha au mwingine apate kipaji cha kuzaliwa hapa Kenya, ye ye asipewa nafasi ya huongozi: Kwa sababu tunawezaja kumpa mamlaka ikiwa tumenyima wale walio wazaliwa wa baba na mama. (inaudible) Kwa upande mwingine wasipewe kazi kwa sababu wakipewa kazi kuna watu wengi ambao hawana kazi, na inawabidi wakeshe kwa baba na mama. Ikiwa kutakuwa nafasi za kazi, kwa hivyo watu wengi au wale watakuwa karibu hawatapata nafasi ya kazi na maisha yao yatakuwa ya taabu. Na wasipewe nafasi ya kumiliki mali ya asili kama ardhi au msitu au kitu chochote wawekewe vikwazo fulani. (inaudible)

Watu kutoka nchi zingine wana pesa kushinda sisi. Kwa hivyo atapewa ardhi hii kwa kuenda kufanya mambo ya kichinichini. Kwa hivyo tunasema

**Com. Mosonik:** Mr. Sholo did you have a memorandam

**Ahmed Sholo :** Nimeandika na I forgot to----(inaudible)

**Councillor Kicheko :** Salaam Aleykum ..

Kwanza nataka kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupatia nafasi kama hii kwa kuja kuchukua maoni kutoka kwa wananchi wenyewe. Fursa kama hii mara nyingi hua siipati. Nashukuru Tume hii kwamba inaweza kufikiria kuchukua maoni direct kutoka kwa wananchi, halafu ipelekwe kwa Bunge ili iweze kutatuliwa. Nina imani kubwa ya kwamba katiba itaweza kutengenezeka kwa haya ambayo tumezungumza.

Kwanza, tunataka tuwe na serikali mbili. Ikiwa ni serikali ya majimbo. Pwani iwe na uongozi wake, na Bara nayo iwe na uongozi wake. Nikizungumza hivyo sisi hatutaweza kupata haki zetu, maana kwa siku nyingi huwa tumetawaliwa na serikali moja lakini hatupati haki zetu, sisi watu wa Pwani. Rasilmali kubwa inatoka Pwani na haitekelezwi ipaswavyo kwa wananchi waliozaliwa Pwani.

Kwa hivyo ninaomba tuwe tunajivunia vitu vyetu vya pwani, na mtu wa pwani awe anaweza kuchaguliwa kuwa Rais. Lazima awe raia wa Kenya, awe na umri usiyopungua miaka thelethini na tano, ateuliwe kwa chama cha kisiasa, ateulewe na watu wasiopungua elf moja kupitia kwa kura. Iwapo ni mtu mmoja tu awezaye kuchaguliwa, kisha mtu huyo ashinde kiti katika sehemu yake ya uchaguzi wa Bunge, katika uchaguzi mkuu, utangazwe kuwa Rais. Rais asiweze kuwa amiri mkuu wa majeshi. Mamlaka ni Bunge au kupitia kwa wananchi. Rais asiweze kuteuwa mawaziri, na manaibu, iwe ikipitia kwa Bunge. Rais asiweze kuteuwa mkuu wa sheria au wakuu wa Tume la uchaguzi au mahakimu, au ma-DC ambao (inaudible) za serikali. Mamlaka hayo ya kuteuwa mabalozi, Rais asipewe uwezo huo, ziwe zateuliwa na Wabunge.

Makamu wa Rais: Ikiwa Rais amejiuuzulu au akiweza kupinduliwa, au akiwa mgonjwa au akiwa amekosa akili. Makamu wa Rais awe anatawala kwa muda wa siku sitini, na uweze kupiga kura baada ya mieze sita hivi, ndio kutateuliwa Rais. Iwapo hakuna makamu wa Rais (inaudible), baraza la Mawaziri liteuwe waziri mmoja ashikilie.

Serikali ya mitaa – Madiwani wawe watakuwa wamesoma kupungua angalau tayari darasa la saba, ili aweze kuhudumia wananchi wake vizuri. Ikiwezekana iende kwa kura ya maoni kwa wananchi wenyewe. Mayor awe akichaguliwa na wananchi, na Chairman awe vile vile akiteuliwa na wananchi, vipindi viwili kwa miaka miwili. Baadaye, anaweza kuteuliwa tena kwa muda wa miaka miwili. Ikiwa hatatekeleza wajibu wake, awe rahisi kutoka, na itapitia kwa kura ya wananchi. Halafu – councillors hao watalipwa ma Central government badala ya local government. Councillors wawe wanalipwa na Central government kama wale wabunge wanaolipwa na serikali. Pale kupitia kulipwa na serikali ya mitaa ndio wananchi inabidi wanyanyaswe kwa kufwata license, kwa mfano lete ndogo ndogo za kula ----- Kwa hivyo tunaomba councillors wawe watalipwa na Central government na (inaudible) ziwe zaenda kwa government.

Katika kupata Passport: badala ya karatasi ya birth ya hao wazizi wawili, sasa imekuwa mpaka upate bank statement ndio uweze kupata passport. Sisi wabajuni hatuna masaa wala hizo bank statements, huwa hatuendi kwenye bank. Kwa sababu mpaka dakika hii serikali haijaweza kutupatia hati za kumiliki, vipi tutaweza kupata passport, ikiwa mpaka tutoe bank statement? Kwa hivyo hiyo hatutaki. Tunataka tuwe tukipata Passport kwa kua raia wa Kenya, na ID yake, na birth ya mama na baba.

Mbunge awe anatembelea eneo lake, au sivyo, kwa muda wa mwaka mmoja atolewe kwa kura ya maoni ya asili mia sitini na tano. Kwa maasilisho ya sheria yapitishwe Bungeni, wajadili, kwa kura ya maoni. Kwa (inaudible) naomba ipitshwe mikoani na kwenye district, kwani wakristo ni wengi sana na wao ndio wabunge.

Sheria za kislamu - sheria za kislamu ziwe zinasikilizwa na waislamu wenyewe. Machief Kadhi wawe wanapewa uwezo wakuhukumu kama Mahakimu wakuu. Chief awe anachaguliwa na wananchi pamoja na manaibu wake. Maana huwa litaondosha tofauti ya kuweza kutawala kimabavu.

(Interjection from the floor): Sawa.

Kuhusu mazingara yetu ambayo tunayo, uvuvi - Tuwe tumepewa uhuru wa kuchukua mali popote na iwe inabakia hapa hapa. Ukulima: Tuwe tutaweza kusimamia mali yetu ya ukulima, na tuweze kupewa sehemu ile ya ardhi ambayo iko na rutuba amba tulikuwa tukiwekewa.

Kuhusu kazi Wakaazi sehemu ile wawe ndio watapewa watoto wao wapate kazi Isiwe sisi ni watu wa Faza lakini kazi ikija si alali ikiwa ni ya Lamu, inanyakuliwa na watu wa Mpeketoni au wa Mombasa au wa Kisumu. Hiyo hatutaki, tunaka wale wakaazi wapate kazi zile.

Wafanyikazi wa serikali – Wasiwe wakipewa kazi za kisiasa zinapotokea kwa mfano za kuesabu watu au kuesabu wapiga kura wapewe vijana wengine amba wamesoma amba hawana kazi. Wafanyakazi: School's boarding fee ilipwe ---- anaweza --- kwa serikali ambayo itawalipa wale wafanyikazi. (yaani subordinate staff) Baada ya yao isiwe kwani headmaster akipewa zile pesa, ye ye humlipa mfanyakazi apendaye ye ye mwenyewe.

Upande wa Bunge – tusiwe tukiongezea mbunge wakati akiwa amechaguliwa kwa kura na hakutekeleza mambo aliyo ahidi kwa miaka miwili. Tuweze kupiga kura ya maoni aondolewe mara moja. Nauliza mnataka serikali hii hii au ya majimbo? (Response ) Hayo ni maoni wanaongezea wakisema wanataka serikali ya majimbo. Hawa wote waliokuja hapa kurekebisha sheria hii huwa watoi maoni yao, wengi wakithania iwe kuna jimbo lao wenyewe, kama walivyo zungumza kutoka wale walinitangulia. Asalaam Aleykum.

**Com. Mosonik :** Nikuuilize swali – wewe ukasema tuwe na uongozi wa pwani, na Rais wa Bara. Ulikuwa unamaanisha nini?

**Councillor Kicheko :** Nilikuwa namaanishaa tuwe na serikali ya majimbo. Tuwe na serikali yetu na serikali ya Bara. Kuanzia huko Taita Taveta kuja huku, ndio tuwe na President, mbunge na councillors wetu, na kule Bara wawe na MPs wao, kama Tanzania bara na Zanzibar.

**Com. Mosonik :** Kwa hivyo hatutakuwa na Rais upande huu?

**Councillor Kicheko :** Upande huu tutakuwa na Rais wetu. Na watu wa Bara watakuwa na President wao. Kama Tanzania Bara na Zanzibar.

**Com. Mosonik :** Kuna President wa Pwani ?

**Councillor Kicheko:** Yes, kama kuna President Zanzibar?

**Com. Mosonik :** Yes.

**Councillor Kicheko:** President ni mainland, kama ni main land kuna --- Kwa hivyo ndio tunasema sisi kila mahali tuwe na President wake na ma-Vice wake.(inaudible)

**Com. Mosonik :** Na sasa umetaka shauri kwamba hawatakuwa na majimbo yao, wako inchi moja? Kuhusu jimbo na hata wengine wawe na majimbo yao. Je unataka kuwaunganisha?

**Councilow Kicheko:** Yaani nataka tuwe na jimbo ili tujiongoze sisi wenyewe, na watu wa Bara wawe na jimbo lao.

**Com. Mosonik :** Kwa hivyo majimbo yatatoka mawili.? Na sasa tutasikia kutoka kwa Walladhu Muhaji. Unataka kusema tuwe na jimbo hapa na watu wa bara watengeze jimbo laovile wataona? Ndiyo hivyo?

**Councillor Walladhu Muhaji:** Jina langu ni Councillor Walladhu Muhaji wa Tchundwa location na ninaakilisha chama cha Safina Party. Langu ni kuwashukuru sana kutupatia wakati kama huu. Katika maoni yangu nimegawa sehemu kumi na moja (inaudible). Kwa hivyo ningewomba tusikilize kwa utulivu kwa sababu wakati niko nao bila haraka yoyote.

Kwanza matibabu na elimu – Serikali ina jukumu itoe elimu na matibabu ya bure kwa wananchi wote, hasa makiba madogo madogo na yaliyo masikini.

Kifungu cha pili: nasema Rais wa Kenya awe na uwezo wa kupokea na kukaribisha wageni wala asiwe juu ya sheria, wala si Mungu. Ashtakiwe kama vile kila mtu anashtakiwa kwa kosa lolote. Asiwe na uwezo wa kuvunja Bunge

Kifungu cha tatu: mimi nasema Bunge letu la Kenya liwe na uwezo na mambo yote yatolewe kwa wajumbe na wasaidizi.

Jeshi letu la Kenya lisimamiwe na Bunge.

Majaji, makatibu, PC, DC, DO Chief na subchief, na watumishi wote wachaguliwe na watu.

Kifungu cha nne : kuhusu Quran –Quran itambuliwe na Katiba. Kwa sababu ndiyo maandishi sahihi kwa waislamu na Mwenyezi. Serikali isijaribu Quran, iheshimu Quran.

Kifungu cha tano: Bwana Chairman nikiendelea – Dini ya Kislamu – Katiba iipe heshima dini ya Kislamu kama ile dini ya Ukristo. Serikali ya Kenya inatambua Jumamosi na Jumapili kama siku za mapumziko. Hii Jumamosi inatoa heshima kwa dini ya kiyahudi. Na hii Jumapili inatoa hesima kwa dini ya Kizungu. Katiba yetu iweke lazima siku ya Ijuma iwe ni siku kamilifu kwa waislamu wote kwa mapumziko. Katiba ishirikishe Sharia Law, itumike. Wanaokataa Sharia Law ya Kislamu ni wale wanaopendelea ufisadi, unyang'anyi, kuuza mali ya watu, kuua watu, na mengine mengi. Sharia ya Kislamu, anayeiba akatwe mkono, mwenye kuua auliwe.

Kuhusu (inaudible) – Sehemu yetu yadhabri dhahabu na lazima tuwe na uhuru kamili kwa kutumia kwa manufaa yetu, Bajuni. (inaudible) yetu, ni mali ya asili imani ya chini ya Wabajuni kuanzia tangu mwezi wa madalao kumi na mbili serikali haina halisi. Kwa sababu serikali imechukua mali kimabavu. Na huu ni ufisadi uliyo wazi. Kuna ufisadi wa watumishi wa umma. Hii iwe chini ya mamlaka ya Bajuni wenywewe.

Kifungu cha sita, naendelea, Polisi – Katika Katiba mpya, lazima Polisi asiwe na uwezo au ruhusa ya kumtenga au kumpiga mhalifu, hata kwa lugha chafu. Haya maneno ya fidia lazima mfanyakazi wa polisi awe mlinda kauli asiwe mvunja sheria. Kama tunavyojua raia wengi wanakufa kwa sababu ya polisi torturing.

Kifungu cha saba, nasema maneno ya Bahari au ya Ardhi. Katiba mpya ipewe uwezo fulani wa kuishi mahala, kuna madini au mali ya asili. Ikiwa yatatakiwa kuchimbwa au kuhifadhiwa. Lazima serikali iwape wananchi halisi haki ya kumiliki ardhi hiyo kabla ya kuchimba au ya ku-preserve.

Bwana Chairman kifungu cha nane – Uhuru wa dini – Yataka iwe wazi kwa watu wote kwamba, uhuru wa dini ni kipawa ambacho Mwenyezi Mungu amewapa wanadamu. Mafumbo ya dini ni kuwa Mungu alikuwa na uwezo wa kukusanya watu wote kwa dini moja. Lakini hakupenda kufanya hivyo kwa sababu alitaka kila moja awe na uhuru katika kuabudu kwake.

(inaudible) Sio serikali yafaa kulinda dini.

Kifungu cha tisa Bwana Chairman – Umilikaji wa Ardhi: swala la ardhi huwa ngumu sana hapa kwetu Kenya. Kwa sababu limeleta matatizo mengi na mafaa. Tatizo katika sehemu nyingi mbali mbali za nchi yetu ya Kenya ni ardhi. Ukosefu au uchache wa ardhi kwa watu wengi umekuwa tatizo sugu la wananchi wengi, hasa wananchi wa mukoa wa Pwani. Kwa mfano katika kisiwa chetu cha Faza island, ambacho hata watu wengi hawajui kijiji chenyewe kinajulikana kama Faza Island. Hii ni sehemu yenye mashamba mengi yenye rutuba na mazao na majumba vitu naya zamani. Kwa muda wa miaka takribani elfu mbili na zaidi. Wenye kijiji hiki hawana kazi inayotambuliwa na serikali. Na hawa, wanyukusaji wanaitwa (inaudible) kwa hivyo sisi ni maskwota katika ardhi yetu.

Bwana Chairman kifungu cha kumi - Mahakama ya Kadhi: kuhusu mahakama, kadhi mkuu awe na Kadhi's High Court. Kadhi awe na mahakama ndogo au katika kiwango cha daraja ya Chief Magistrate. Kadhi mkuu awe nadaraja ya Judge wa High Court. Kadhi yejote awe na uhuru ya kusikiliza kesi yejote kulingana na uwezo wake. Kesi ikiamuliwa na mahakama ndogo ya Kadhi, inaenda appeal kwa mahakama makuu ya Kadhi. Mumeelewa?

**Com. Mosonik:** Tumelewa.

**Councillor Walladhu Muhaji :** Kifungu cha kumi na moja Bwana Chairman, Haki za kifo: Maoni yangu ninapendelea nchi yetu ya Kenya kupatia usawa katika utumiyaji na kula matunda ya uhuru wetu, kwa wananchi wote. Kila wilaya wananchi wake halisi wafaidike na hayo mawili yanawezekana kupatikana.

Ikiwa, kila kitu ikidaiwa na wananchi wenyewe, kwa hivyo napendekeza Serikali iwe ya Majimbo. Katika utawala wa majimbo lazima mkuu wa jimbo achaguliwe na raia. Wageni ambao si wananchi wasiwe na haki za kuchaguliwa au kuchagua. Na vile vile wageni wasiopatiwa uraia wakusajiliwa kwa karatasi wasiwe na uwezo wa kuchaguliwa kuwa viongozi wa wadhifa wowote hata wa headmen au head-women.

**Com. Mosonik :** Maliza---

**Councillor Walladhu Muhaji :** Bwana Chairman namaliza. Nikifwatilisha kwa jimbo: lazima wafwasi wa dini mbali mbali watiliwe maanani katika Jimbo au majimbo ambayo Waislamu ni wengi sharia ya Islam lazima ifwatwe. Kwa sababu gani? Ili kukomesha ujisadi, wizi na maafa mengine. Mkubwa wa jimbo lazima awe Muislamu, au Makamu wake lazima awe Muislamu. Katika Jimbo au Majimbo wasiyo kuwa Waislamu, mtawala wa jimbo mkuu lazima awe Mkristu. Majimbo ndio mfumo wa kipekee wenyе kuleta maendeleo na mafanikio kwa wananchi. Lazima maafisa wote, watumishi wa uma, wawe wametoka katika wilaya hiyo: Kuanzia Wakuu wa wilaya, maafisa wa elimu, maafisa wa samaki, maafisa wa ukulima, Provincial Commissioner, na ma-DOs, lazima watoke katika jimbo hilo hilo. Wananchi wenyewe kwa wenyewe sio kuletewa.

(Inaudible) kama tunavyojuwa Bwana Chairman, kulingana na serikali yetu ya Kenya inavyoendelea, utumishi wa Urais utajulikana. Kwa hivyo, nasema Bwana Chairman, kama tunavyojuwa Bunge la East Africa limebuniwa na wako na waziri. Lazima wanasema wananchi hao watatu - - Kenya, Uganda na Tanzania - - wasiende kupewa Passport, iwe ni ID. i.e ID iwe ndio passport. Mukenya atikoka hapa kwenda Tanzania, badala ya kuonyesha passport iwe ni ID. Mshaelewa? (Response)

Kwa hivyo Bwana Chairman tafadhali naomba kuongeza – Kuwa Constitution yetu ya Kenya baada ya miaka ishirini na tano (after twenty-five years) ifanyiwe upakuzi yaani ipigwe msasa, iangaliwe kulingana na wakati. Kwa sababu ninaenda. Kwa hayo asante sana.

**Com. Mosonik :** Kuna kidogo hatukuelewa, ulisemaji kuhusu Biwott?

**Councillor Walladhu Muhaji:** Asante sana Mr. Chairman. Kuwa juzi kulifanyika uchaguzi wa KANU Nairobi, mambo yale yalikuwa, japo sikuweza kwenda Kasarani Biwott ndiye mfwasi sana, such that we cannot do without him kwa KANU. Kwa hivyo ningetaka ku add kwa mabashiryo yangu kuwa kuna mambo fulani vice-chairmen wale wamewekelewa, lakini huyo vice-chairman halisi ni Biwott there.

**Com. Mosonik :** Lakini tusikilizane kwamba hilo jambo haliko kwa maswala ya kurekebisha Katiba. Okay, asante.

**Councillor Walladhu Muhaji:** Okay, asante sana.

**Com. Mosonik :** Okay, sasa tumsikilize kwa ufupi, hebu ufupishe, Haji Chola Walla, ye ye akiwa nje tutapata mwingine. Kwa sababu kuna Halima Dido, Kuna Halima Dido? Halima Dido yuko na ana memorandum atatupa baadaye.

**Halima Dido :** Asalaam aleikum. Mimi hapa niko na maoni ya youth kuhusu marekebisho ya Katiba. Jina langu naitwa Halima Dido. Na katika topic ya kwanza kuna maoni ya youth kuhusu uraia.

Number one : wanapendekeza kuwa ye yeyote ambaye atazaliwa na wazazi wawili wa Kenya, awe raia halisi wa Kenya.  
Number two: ye yeyote ambaye atazaliwa Kenya na mzazi mmoja wa Kenya, awe raia halisi wa Kenya. Number three: mume au mke awe raia wa Kenya, baada ya kuoana ikiwa mmoja wao ni mgeni. Number four: raia apewe huduma zote za kimaisha kama vile - elimu, afya, makao, usalama, chakula na uhuru wa kuzungumza. Number five: raia awe na jukumu la uchungaji sheria, kama: kuchunga usalama, kuchunga mali asili. Number six: haki na jukumu ya raia yategemeenamna uraia ulivyopatikana. Number seven: raia wa kuzaliwa awe na nafasi zaidi kuliko raia wengine. Number eight: Katiba isiruhusu uraia wa nchi mbili. Number nine,: Wakenya wawe na vitambulisho kwa mfano, kitambulisho cha kitaifa na karatasi ya kuzaliwa.

Topic ya pili – Hawa youth walikuwa na maoni kuhusu elimu. Number one: walipendelea kuwa elimu ya msingi iwe bure na serikali ichukue mamlaka ya kutoa vifaa vyote vinavyohitajika kwa mfano - - text books, exercise books and games items. Number two: shule za msingi katika sehemu za Waislamu ziwe na kipindi kimoja tu, that is, iwe na one session. Number three: masoma yapunguzwe katika shule za msingi. Number four: mfumo wa elimu urekebishwe badala ya 8-4-4 iwe 7-4-2-3. Number tano: fees zipunguzwe siwe za kiwango cha chini. Number six: Katiba ichukue jukumu la kuwaajiri wale waliomaliza kidato cha nne. Number seven: Katiba ichukue majukumu kutoa mafunzo ya Vyuo Vikuu, i.e colleges bure, na pindi wanapofuzu kipindi cha kusoma kwao wapewe kazi bila kuchelewa. Number eight: Katiba ihakikishe kuwa watu wanaoopata nafasi ya vyuo vikuu, that is university, wasome bure na walipe garama baada ya kupata kazi. Haya yalikuwa ni maoni ya youth kuhusu elimu na uraia. Shukrani.

**Com. Mosonik :** Nataka kuuliza, Halima amesema shule (inaudible). Hujatueleza kwa nini.

**Halima Dido:** Walikuwa wanapendelea kuwa shule za msingi katika sehemu za Waislamu ziwe na kipindi kimoja tu, that is one session. Walikuwa wamenieleza kuwa, saa hii wanaenda shule kutoka za mbili mpaka saa sita na nusu. Sasa walikuwa wamesema kutoka saa nane mpaka saa kumi. Hiyo section ichukuliwe na masomo ya kidini. Kwa hivyo itakuwa ni shule wamesoma kwa kipindi kimoja tu cha ukufuru. Asante.

**Com. Mosonik:** Umesema wababilishe mfumo wa 8-4-4 warudie ya zamani. Sasa swal, tunarudi nyuma ama tunaenda mbele?

**Halima Dido :** Hii walikuwa wamenieleza ya kwamba. Hii system iliyoko sasa ni ya miaka minane primary school, miaka minne secondary school, halafu miaka minne university, if I am not wrong. Sasa walikuwa wamesema iwe 7-4-2-3. Kwa sababu ikiwa hivyo, hapa hali ya masomo itakuwa inapanda kila wakiendelea mbele.

**Com. Mosonik :** Pengine nataka ueleze kwa sababu  $8 + 4 = 12$  and  $7+4 = 11 + 2 = 13 + 3 = 16$ . Yaani kwa system hii ni kwamba watoto wasoma miaka minane na tena Chuo kikuu wasoma miaka minne. Kwa maoni yangu binafsi ni kwamba ni afadhali chuo kikuu wasome miaka minne kuliko miaka mitatu. Kwa hivyo masoma ya juu, lakini tuna ----- (interjection which is inaudible)

**Halima Dido :** Iko Faza location, ya

**Com. Mosonik :** Sasa tuelezee majina halafu uendelee.

**Ahmed Hassan** - Kwa majina mimi naitwa Ahmed Hassani na ni mwalimu. Jana tulikuwa na discussion na wakatoa

suggestion kama hizo. Kwa hakika walisema huu mfumo wa 8-4.-4, ya eight years primary school, four years secondary or ‘O` Level and four years university, huwanyima nafasi. Kwa mfano kama ukitoka form four, watoto wengi hukaa nje, na tunajua kwamba serikali yetu ya Kenya hii sasa haiajiri watu. Hata tukifanya bidii tukienda ma-college watu wanatoka bila kazi. Lakini tukipata ile two years tukijiendelezha itakuwa ni nafasi kubwa kwa watu, badala ya kupotea na kwenda kufanya mambo ambayo hayataki ka katika nchi, wawe wanaendelea na kusoma. Kwa sababu si rahisi, hivi sasa wanapomaliza masecondary ni wengi sana. Lakini wanavyopata nafasi ya kwenda chuo kikuu ni wachache sana. Lakini ikiweko two years shauri ya A level, itakuwa ni rahisi. Kwa sababu, ukikumbuka siku za nyuma, sehemu nyingi zilikuwa na high schools. Lakini sasa hakuna. Utaona ndio wasomi wengi wamekosa nafasi, na washerati, ujisadi na madhambi ya kila aina yanatokea. Kwa sababu wafwata masomo na hakuna kazi. Wakiendelea na Form five na Form six, hatia zile zinapungua. Lakini kwa hapo mmefahamu vizuri.

**Com. Mosonik :** Tausi Madinya,

**Speaker from the floor:** Nafikiri ameenda.

**Com. Mosonik :** Okay kuna councillor, no, Imam Hatma Suleiman na ufupishe tafadhali.

**Hatma Suleiman:** Salaam Aleykum-----Mimi jina langu ni Hatma Suleiman wa Kizingitini hapo ni karibu ---.

Mimi katika mambo yangu ni kwamba uchumi wetu wa Lamu Mashariki ni wa mikoko. Kwa hivyo twaomba mikoko ifunguliwe nchini iwe atauzwa kwa mikoko hata ya nje, kama namna ilikuwa inatunzwa wakati wa Khayati Rais Kenyatta.

Jambo la pili: sisi watu wa Lamu Mashariki hatuna umilikaji wa ardhi. Kwa hivyo tunaishi kama wageni. Tunataka tupatiwe umilkaji wa ardhi kama wananchi wengine katika Kenya hii.

Tatu: sisi watu wa Lamu Mashariki uchumi wetu ni wabahari. Kwa hivyo tunaomba kwamba kila kinachotokana na hii kiwekwe ruhusa ya kutumiwa kama sasa na kwa sababu ndio uchumi wetu sisi watu wa Pwani au sisi watu wa Lamu Mashariki. Vile vile sisi watu wa Lamu Mashariki tu watu bahari, tuingie sana bahari. Tunaomba kazi yote inayohusika bahari kama ya navy au kama ya kuzamia, tupatiwe sisi watu ambao kazi hiyo ndio kazi. Kama Wabara wakiwa ni watu kumi na wa pwani wawe kumi katika hilo jahazi au meli.

Lingine: sisi Waislamu tunataka mambo yetu ya Kislamu iende kisheria ya kislamu bila ya kuguswa chochote yeoyote au kupunguzwa chochote.

Sisi watu wa Lamu Mashariki tunashida ya matibabu kwa ukosefu wa vifaa na madakitari wa juu na usafirishaji. Iwapo kutatokea hatari kwa mgonjwa, kwa sababu ya uzazi au mengineo, tunashindwa. Huenda mtu yule atafariki, ilhali kwamba

inawezekana mtu hakufariki, lakini kwa ukosefu wa vifaa anafariki. Kwa hivyo tunaomba jambo kama hili lisahisishwe.

Hiyo nyingine – twaomba katika mashule yetu yote ya Kiislamu, wapatikane ndani yake waalimu wa kidini, ili watufunze dini.

Mhalifu: yejote anayepatikana na wakosa asitoe hongo, kule kutozwa hongo ndio makosa ya uhalifu kama ule. Kule kutoa hongo ndio kuzidi makosa kwa mhalifu kama huyo. Kwa hivyo isiendelee hongo.

Jambo lingine ni kwamba: mawasiliano ya kisimu au ya aina nyingine, tusahihishiwe, tunaomba maana jambo likitokea lolote, iwe ni haraka jambo kama hilo kujulikana au kupatikaniwa tukasaidiwa.

Hilo nyingine: masikini, mayatima, viwete, madhaifu, watahudumiwa bure, kama mama aangaliavyo binadamu wengine. Waangaliwe vizuri.

**Hatma Suleiman:** Waagaliwe vizuri: wapewe chakula ili waweze kuishi katika Kenya hii kama mtu yejote ambaye ni Mkenya.

Pia la mwisho, mtu yejote ambaye yeje ni mgeni asipatiwe madaraka ya kuweza kuongoza ili kumtosheleza mzaliwa katika nchi kama hii. Kwa hivi mgeni kama huyo leo atapata madaraka, itakuwa amemunyima haki mzaliwa. Kwa hivyo tunaomba jambo kama hili lisipatikane. Wasalaam Aleykum wa Rahmatulilahi Wabarakatu.

**Com. Mosonik :** Sasa tumsikilize Ali Kidadi – business man

**Ali Kidadi:** Salaam Aleykum. Mimi naitwa Ali Kidadi, mkaazi wa Faza. Makamishna nataka kuguzia, Rights of a woman – Haki za mwanamke wa Kenya. Na kwa ufupi sana Bwana Commissioner, hii Katiba yetu tulio nayo sisi hapa Kenya ambayo tunaifanya marekebisho, tulifundishwa na mkoloni namna ya kufanya. Hao pia walikuwa wamefanya Katiba zao nyingi, na katika hizo Katiba zao tunaweza kuona wazi wazi wamemdhumu mwanamke. Sasa sisi tukifwata mfumo ule ule tunaweza kuona kwamba mwanamke amedhulumika sana. Kwa hivyo ni maoni yangu Katiba mara hii, pindi kamilika liangaliwe sana swali la mwanamke. Makamishnas nikiwapa mfano. kama mimi mfano naitwa Ali Kidadi, na ndugu yangu mwagine aitwa Zainabu Kidadi. Sasa mimi naona kutoa mke wangu kutoka nje popote serikali hii ya Kenya inamheshimu mke wangu zaidi, kwa sababu huenda ikampa uraia bila taabu.

Lakini nikiangalia vile ndugu yangu wa kike, ambaye ana the same right, yaani yeje mama yake, baba yake, na babu yake hawana tofauti kabisa na mimi, hana haki kamwe. Ikiwa ataolewa, akileta bwanake hapa Kenya, hapati uraia. Huwa nidharubu kali sana. Je hii ni haki? Nikikupa mfano Bwana Commissioner, kutokana na hawa wanawake wa Kenya angalia mahali ambao wanafanya kazi au wanasoma. Sasa huyu msichana ame-pass amepatiwa university kule America, Uingereza, au kwingineko. Utaenda kuona hana haki kujitilia saini binafsi - - ndio Kenya - - katika visa mpaka amlete babake, si ni

dhulumma? Ikiwa dhulumma kama hii itaendelea tutafika wapi? Sasa twasema tunataka usawa, haki za binadamu ndio hii tunamaanisha. Utaona mwanamume, hati kama hiyo yeye hupewa mara moja, anapewa Visa anatia saini na mambo yake yanakwisha.

Swala lingine Bwana Commissioner, kubwa kwa mwanamke wa Kenya. Mwanamke anayefanya kazi kwa madaraka yoyote hapa Kenya akipewa transfer mara mbili - - kuna kita inaitwa disturbance allowance yaani ile kusumbuliwa sumbuliwa ukipelekwa hapa na pale - - mwanamke wa Kenya hio apewi kabisa. Hii napenda kuona kwamba nidhuluma. Kwa sababu yeye ,wanamke yule yule anafanya kazi kama huyo mwanaume. Lakini kwa sababu ya ule ubaguzi tuli nao ambao anatoka nyuma na kumdhara mwanamke, twaendelea kungandamiza.

Kwa hivyo Bwana Commissioner, nimezileta kwa hii Katiba mpya ambayo tumejitolea kuirekebisha maoni kama haya yangu yaangaliwe vizuri sana. Nikirudia kwa ufupi: mwanamke yejote ambaye ameolewa - - kwa sababu hana haki yeye kama mume - - akiolewa na mumewe pia awe na hiyo haki moja kwa moja bila kusumbuliwa. Kama mimi leo nataka kuo, nikija na mke wangu hapa Kenya anakua raia, kwa nini mwanamke asiwe hivyo? Kwa sababu yeye anaolewa na mwanaume wa nchi nyingine, ukimchukua ampeleke kwao huyu mwanamke ni mwananchi. Au mwanamke wa kuko akiolewa na bwana wa huku, pia anakuwa raia. Na nchi nyingine pia utakavyoona kwa hali ya ubinadamu, wewe ni refugee umekwenda kule lakini umezaa watoto, yule mtoto kuzaliwa pande ile tayari amekwisha sajiliwa uraia kwa wazazi wake wote. Kwa sababu, haiwezekani mtoto yule aleewe vizuri kama hatakuwa na uhusiano na wazazi walili. Kwa hayo asante sana.

**Com. Mosonik :** Asante. Haji Shilu. Hayuko? Mohamed Omar

**Mohamed Omar :** Bwana Makamishna, DO wetu, wafanyakazi wasaidizi wa hii commission, viongozi na wote mabibi na mabwana, Salaam Aleykum. Jina langu ni Mohamed Omar Abdallah na ninafanya kazi na hii commission, mwanakamati wa Lamu Mashariki. Yangu mimi pengine yatakuwa machache, kwa sababu nilipewa maoni ambayo ni wasilishe kwa hii commission na watu ambao hawakuweza kufika mahali kama hapa. Kwa hivyo ikiwa mapendeleo ya Commission nisome maoni haya, basi nitaendelea. La wakiona haitakuwa sawa niwaakilishe kwa Commission, basi nitawakabithi hiyo Commission.

**Com. Mosonik :** Tafadhali uyasome.

**Mohamed Omar:** Asante. Mapendekezo ya kuasilisha kwa Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya, yaani kwa ufupi CKRC. Wasema “sisi watu tunaoishi katika kijiji cha Siu, tarafa ya Faza, wilaya ya Lamu, tunamapendekezo yafwatayo kuhusu maswala tofauti tofauti”: (Hapa nitataja maswali matano). Ikiwa moja wapo ni: swali la Ardhi, sheria za kidini, elimu, afya na uchaguzi.

Swala la ardhi, wameeleza hivi. Sisi ni watu ambao tumeishi katika upande wa pwani, tumetakikana wandugu zetu walioishi

pwani kwa karne nyingi zilizopita ziwezi hesabika. Waliomiliki ardhi za Lamu wakawa na mashamba, tukajenga manyumba ambayo kwamba hata watu kadha wanaokuja kututembelea ili katuona wakaribishwa majumba hayo yaliojengwa wakati huo. Kwa hivyo, hivi ni kusema kuwa sisi ni wananchi wa Kenya wa kuzaliwa hapa nchini, bila shaka yoyote. Uraia wetu hauwezi kutiliwa shaka na yeyote. Lakini wanaeleza masikitiko yao wakisema kuwa “tunashangazwa sana kuwa baada ya wazee wetu kukaa kwa muda murefu na sisi kukaa kwa muda wote huo, kila unapomba vyeti nya kumiliki ardhi, huwa hatupewi. Wanasema, “tupendekeza ya kuwa: serikali itambue ardhi hiyo kwa milki yetu, kila mmoja apewe cheti cha kumiliki ardhi. Haki itekelezwe kwa wote kwa sababu bila vyeti nya kumiliki ardhi, yaani Title Deeds, tunaweza kuzikosa hizo haki zetu.

Sheria za kidini – Wasama maswala yote ya kuhusiana na dini ya Kislamu yamuliwe na Makadhi. Sheria ya mtu kuchaguliwa kwa Kadhi ibadilishwe yaani mfumo amba o uko hivi sasa ubadilishwe. Wanasema.” Kadhi awe anachaguliwa: mtu mwenye elimu ya dini ya kutosha, yaani awe mwanachuoni, awe sifa ya uaminivu, na mwendo mzuri kwa jumla. Sheria ya sasa yasisitiza zaidi mtu awe amemaliza kidato cha nne, yaani Form four, na pengine hana elimu ya dini ya kutosha ya kuweza kutatua maswala kama yale ya urathi, talaka na maswali mengineo muhimu. Pia wanasema, ”iundwe kamati ya wanachuoni kutoka pande zote ya Kenya, ili wafanye mahusiano kwa wale wanaopeleka maombi ya kuomba nafasi za Makadhi. Wanasema kuwa, “watakaopitishwa na wanavyuoni – yaani Masheikh, basi majina yao yakabidhiwe serikali, na watambue hao kama ni Makadhi, waliochaguliwa na Masheikh wa Kislamu, bila ya kubadilishwa lugha hiyo. Kwa hivyo Rais awe hana uwezo kabadilisha, isipokuwa afwabilia yale maagizo ya Masheikh walioamua. Wasema “serikali itambue Kadhi kuwa ni hakimu kama hakimu mwingine serikalini - - anapoamua kesi za Waislamu mtu asiwe na uwezo wa kwenda kupinga uamuzi huo katika koti nyingine yeyote, yaani tusiwe na uvezokano wa koti ya kuwa na appeal kwa mahakama nyingine isipokuwa za sheria za Kislamu.

Elimu – Wanaeleza kuwa “elimu ya msingi kwote nchini itolewe bure, yaani free primary education. Wanaeleza kuwa “mzigo wa karo za shule husababisha wazazi wengi kuwakatiza masomo watoto wao.

Swala afya – Wanasema” kila tarafa kuwe na hospitali yenyе vifaa nya kisasa na madakitari wa kutosha. Kwenda katika hospitali za wilaya yaani District hospitals, kutafuta matibabu ni jambo gumu. Wanaeleza kuwa, “kutafuta matibabu ni jambo gumu, na shida za usafiri kulinganisha na mahali ambapo sisi tunaishi. Kwa hivyo wanapendekeza kwamba wagonjwa wanapopelekwa mahospitalini kwa kuchukuliwa mbali kwa hospitali, na vile hospitali haiko karibu, kwa kuwa zilizopo hazina vifaa nya kutosha, basi wagonjwa wao pengine hufariki kabla hawajafika huko hospitalini. Kwa hivyo zile zahanati, yaani health centres ambazo ziko katika kila tarafa ziimishwe.

Swala la uchaguzi – Wanasema, “raia wanaopiga kura ya kuchagua Mbunge atakaye waakilisha Bungeni, wawe na uwezo wa kupiga kura ya kutokuwa na imani na mbunge huyo iwapo hashugulikii masilahi yao. Kura ya kutokuwa na imani na mbunge ipigwe miaka miwili baada ya kuchaguliwa kwa mbunge huyo. Wanapendekeza kuwa, “uchaguzi mdogo uitishwe kujaza nafasi ya mbunge huyo, tuseme ambaye pengine amechaguliwa na hatamani tena kurudi kwao mpaka baada ya miaka mitano.

Kwa hivyo hayo kwa jumla ndio mambo ambayo wameandika katika mapendekezo haya. Na ninashukuru Bwana Commissioner kwa kunipatia nafasi kama hii kuweza kusoma maoni kama haya. Nashukuru, asante.

**Com. Mosonik :** Asante, nauliza kama Zuena Mahamed alirudi? Je kuna mtu yejote ambaye hakujandikisha na angependa kutoa maoni saa hii? Kila mtu ametoa maoni yake? Ulikuwa umetoa maoni yako? Kwa ajili gani hukujandikisha? Saa hizi? Up till hii saa ya mwisho. Yes wa mwisho kabisa ni Ali abdalla Sikanga, please – individual oral submission.

Chukuwa microphone, ni wewe?

**Ali Abdalla:** Yes

**Com. Mosonik :** Chukuwa microphone na sema umalize dakika tano, usizidishe, halafu uje ujiandikishe hapo, please.

**Ali Abdalla Sikanga:** Salaam Aleykum...Jina langu naitwa Ali Abdalla Sikanga. Niko na maoni ile ya Katiba ambayo itakuwa ikibadilishwa katika nchi yetu ya Kenya.

Maoni yangu ningependa: Katiba iende ikajue ama ikajulishe hali iliyokuwa kabla ya leo. Baada ya hapo ihakikishie au ijulishe kila mwananchi, wa sehemu, kila aliyeusika katika nchi yetu ya Kenya. Baada ya kujulisha Katiba iliyopita na kujulikana mikataba ile huenda kuwekwa, ya watu au ya binadamu aliyeuweko kabla ya sisi leo ambaye ndiye ametamalaki nchi kama hii.

Baada ya hiyo Katiba kwenda kufahamishwa kwa kila moja wetu, agreement ama ule uandishi ama mkataba ule wendakuwekwa, baina ya waliokuwa wanaishi katika hizo sehemu, na waliokwenda kuchukua yale madaraka, ilikuwa ni ipi? Baada ya kila mwnanchi amekwenda kufahamu na kuhakikishiwa katika akili yake bila ya udanganyifu, hakika iliyoandikishwa, na kujulikane ni kasoro gani iliyokwenda kupitika au iliyoendelea, kwa kutakakikana hiyo Katiba ibadilishwe leo hii.

Mwanadamu ni kiumbe aliyeletwa ulimwenguni. Mwanadamu leo hii anaweza kwenda kuunda gari, tiari au anaweza kufanya mpango wa kifaa chochote kama tunavyozunguza katika vifaa hivi hapa. Ataweka sehemu kwamba hii itumiwe namna hii. Kwa gari kwamba hapa uweke (inaudible), hapa uweke oil, hapa ufunge grease, na hapa uweke maji. Utakapotumia kulingana na zile sharti ulizozieka katika chombo kama kile, ukazifwata kwa njia inayostahili, hakika yake kile chombo utaishi nacho wakati ulipotarajia ulipokiunda. Hivyo hivyo Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba mwanadamu leo hii.

Kwa hivyo, Katiba au sheria ya huyu kiumbe aliyweweka na yule aliyemuumba ni ile ile iliyomuwekea. Ndugu zanguni binadamu, Mwenyezi Mungu amekwenda kutuvekeea sisi, kuwa ni viumbi vitukufu katika ardhi kama hii. Akatuwekeea taratiba

ya kuitamalaki ama ya kuiendesha ardhi kama hii au ulimwengu. Tunaweza kusema kwa jumla, ulimwengu umetamalakiwa na mwanadamu. Akitaka kuweza kufwata njia taratibu au ile mifumo aliyowekewa na yule aliyemleta katika ulimwengu huu, hakika yake ni kwamba atakwenda kufaulu, na hapatapatikana kasoro ama umwajikaji wa damu, ama kasumba zote kinyume na taratibu. Mfano wake narudi katika gari: utakapokwenda kuchukua sehemu ya petroli ukaweka maji, ndugu yangu ile gari sidhani kama unaweza kwenda nayo.

Hivyo hivyo tutakapokwenda kuichukua sheria au mfumo tuliowekewa na yule aliyetuweka katika ulimwengu huu au ardhi hii hapa sasa tulipo, tukaenda kinyume nayo ndugu yangu umehathirika. Mfano mdogo ukaja ukamkosea mtu au ukumpiga kofi, pengine maisha yako yawe yakaondoka saa hio hio. Ndugu zangu binadamu, kwamba Katiba ama sheria ni mfumo wa huyu mwanadamu atakayeiweka kwa kutumia taratibi zile zile alizowekewa na aliymueka.

Sasa kwa ufupi ndugu zanguni, maana inaweza kuwa ni mbegu kulingana na muda niliyopatiwa ni kidogo - - -.

#### **Com. Mosonik : Maliza**

**Ali Abdalla :** Sasa kwa ufupi naweza kumalizia nikisema, kwamba sheria ya huyu mwanadamu au Katiba, ni ile iliyokuweko tangu hapo mwanzo. Kwa mwanadamu kijihe (inaudible) ni muhimu. Tunafahamu baba yetu Adamu mpaka mtume wa mwisho, na karibu wa mwisho nabii Musa, ambayeni Moses, nabii Isa ambaye ni Yesu na Mohamed ndio wa mwisho, hio Katiba ndio ambayo mwanadamu anafaa hifwate.

Kwa ufupi, kwa kufungia hotuba, ninapendelea kwamba ule mfumo ama Katiba iliyokuweko - -Mkataba - - udhihirishwe na uonyeshe makosa gani yaliyoyokwenda kupidika, na ni mahali gani panataka kurekebishwa leo hii. Hapana shaka hio Katiba ilikuwa iko katika mfumo wamwanadamu atakaoendelea nao, kwamba imekwenda kuharibika ama kukoseka. Baada ya kuwa kumekoseka, ni kwa leo hii mwanadamu anataka kuleta - - njia gani mimi niyarekebishe yale makosa yangu? Nayo ni kwamba anataka kwenda kuweka mradi. Ni vipi kwa hivyo Katiba itarekebishwa? Hapana shaka, patakuwa ni pale mwanadamu alipokwenda makosa napo, leo amekwenda kusema hapa na lipate kuendelea lile kosa lake,kama limekuwa sahihi. Mfano tumesema pombe ni halali, na ndio Mwenyezi Mungu akasema—

**Com. Mosonik :** Excuse me can you finish now. Ummalize.

**Ali Abdalla :** Wakati ndugu zanguni umeniishia na ni kwamba Katiba iliyoko ni ile ile ,pasipokuwa ni kwamba sheria ichungwe na tuifwate ililiyo miadili ya sheria. Asante.

**Com. Mosonik :** Asante, asante Ali Abdalla Sikanga na sasa nitasimama na kusema kwa niaba ya mwenzangu Commissioner Ahmed Isaak Hassan, amepatwa na Malaria kidogo ndio hakurudi na akaomba msamaha kwa kutorudi. Kwa niaba yake na

wenzangu hapa wote kutoka kwa Tume la Kurekebisha Katiba ya Kenya, nawashukuru sana, sana, kwa kuhudhuria kikao hiki cha leo, kwa kutoa maoni yenu kinaganaga. Tumeyasikia kwa makini, tumeyaandika mnaona vizuri nime andika mimi. Asha hapa anaandika shorthand. Tunaweka tena kwa hii tape, na machine yenyewe iko pale. Kwa hivyo, tumeyasikia kwa makini, tumeyachukua. Tutayawasilisha kwa Tume tukirudi Nairobi.

Tumewashukuru, tena mumesikia kwamba sisi hatukuwa tumekuja area hii hata mmoja. Hakuna mmoja wetu amewahi kuwa area hii. Sasa tumefurahi tena kwa kujua area hii. Nitaomba Bwana DO wa sehemu hii to give a vote of thanks, halafu tutaalika mtu mmoja atufungie kwa maombi.

**Bwana DO :** Asante sana Dr. Arap Korir. Ningechukua hi fursa kupeana shukurani zangu kwa Commissioners wote, wageni ambao waliandamana nao, kuja kututembelea Faza Island, ambayo Faza na Kizingitini. Mmekuja kwa Waswahili, na Waswahili wenyewe walisema: mstahimilivu hula mbivu. Nimejua mlitoka Lamu asubuhi, mkapambana na amri ya maji, kwa sababu hilo ni tegemeo letu. Na mimi kwa niaba ya wananchi wa Faza na Kizingitini, ningependa kupeana shukrani zangu kwa hiyo kazi yote nzuri ambayo mmefanya. Wananchi wametoa maoni, na mpaka saa hizi tunaangalia Commissioners wangali hapa infgawa sasa maoni yameisha. Nafikiria wakati wenyewe mtakua na safari zenu, mkienda sehemu zingine, nimejua kesho mko na jukumu la kwenda Kiunga, lile lenye nitasema ni kwamba muwe na safari njema. Nimejua ni mara yenu ya kwanza kuja Faza na Kizingitini, msiogope maji. Wakati mwingine mtembee muje tukae na tukule vile sisi wenyewe Waswahili huku tunakaa .

Shukrani zangu za pili, zimeenda kwa wananchi wenyewe wa Faza na Kizingiti. Unajua usafiri ni wa shida, lakini tumepata maoni kutoka Faza, Siu ambavyo ni vijiji vilivyo mbali. Kwa huo uvumilivu wenu, nasema asanteni sana.

Shukrani zangu za tatu zinaenda kwa kamati ya Katiba, Lamu East, kwa hiyo kazi yote nzuri wamekuwa nayo kuanzia civic education, mpaka pale tumefikia. Hayo yote yamepitia kwa maoni ya wananchi. Yaonekana ile kamati pia, ilifanya kazi nzuri.

Shukrani zangu zinaenda kwa Provincial Administration, ambapo tuko na chiefs na assistant chiefs, kwa facilitation ya hii meeting. Tuendelee na hii kazi nzuri, na ninafikiria pengine tukiendelea mbele tusiangularie maswala ya malipo bali tujenge Kenya ambayo ni nzuri na itakuwa ni nzuri kwa vizazi vijavyo.

Shukrani ya mwisho inaenda kwa headmaster, Faza Secondary, kwa kutukubalia kufanya mkutano wetu wa Katiba, wahii Tume ya Katiba, hapa kwa shule yao.

Kabla sijamaliza, ningependa kuita Dr. Arap Korir aongee neno moja ili tufunge mkutano.

**Com. Dr. Mosonik Arap Korir :** Nakumbuka nilisema kua mimi hufunza historia kwenye Chuo Kikuu. Kusema kweli, tulikuwa tunesoma tangu mwanzo wa shule halafu tukaanza kufunza katika Chuo kikuu historia ya sehemu hii, na tunasikia

kama hadithi. Kwamba ninyi watu wa hapa malikuwa na civilization yenu na malikua hapa tangu zama za kale. Unajua sisi watu wa Bara tukija hapa hatutakiwi kusema Kiswahili sana, tunaogopa kidogo. Lakini ile historia nimesema kuhusu hapa ni kweli, hata mimi ninajua. Kwa hivyo njia ya kuthibitisha ayo ndio inatakiwa sasa Katiba iangalie na iatengenezwe.

Kitu kingine ni kwamba sisi tumekusanya maoni leo, na tulisema baada ya hapo, tutazunguka Kenya nzima, mkawa number two kwa mikoa. Tulifwata herufi za alphabet Kingereza, kama: a, b, c, d---. Sasa tukaanza na Central, tukaja Coast, tutaenda Eastern wiki ijayo, halafu Nairobi province, baadaye, North Eastern, halafu Nyanza, halafu Rift Valley, tunamalizia Western Province, pengine mwanzo wa mwezi wa nane. Kwa hivyo nyinyi mmefanya yenu vile ilitakiwa kutoa maoni hapa.

Tutakusanya maoni kwa mikoa yote, kwa kila Constituency, halafu tutalinganisha ndio tujue mahitaji ya Wakenya wote. Lakini mfahamu kwamba baada ya kuandika hicho kitabu, Katiba mpya, tutaenda kwa mkutano wa taifa wa kurekebisha Katiba. Vile tulikuwa tumesema. Huu mkutano unaitwa National Constitutional Conference. Kabla ya kwenda mkutano huo tutoa report yetu.

Report kuhusu vile tulifanya kazi: tutasema tulikuwa Faza, tarehe mbili, mwezi wa tano. Tukawakuta wananchi, ndio tulikuwa tukisema mujiandikishe wote hata wale observers waseme walikuwa hapo. Tutaandika report itakayokuwa kitabu kikubwa. Halafu tuseme, kulingana na report vile wananchi walisema, sasa tunafikiria kwamba Katiba iwe namna hii.

Hiyo Katiba itakuwa ni recommendation ya Commission kwa conference. Tukiwa tumeyatarisha maoni, tutaweka kwa Kenya Gazette. Kwa mfano kwa maneno ya harusi ya kanisa ya Kikristu wanasema kuna siku 21 ambazo zinawekwa kwa ukuta. Sasa mtu yejote ambaye ana chochote cha kusema, aseme, ama sivyo, for ever asiseme, mnajua. Kwa hivyo hata tukiwa tumeandika hiyo report yetu na Katiba ile mpya, tunasema: kwa maoni ya Tume, vile raia walisema, tutaweka kama Gazette Notice. Inatakiwa kwanza ziwe siku sitini, hiyo Gazette Notice. Hivyo nikusema mnapata nakala ya report, na mnafungua page yenu, ukurasa, pengine ni mia saba hivii mpaka mia saba na nane, kuhusu hapa, muone kama ni kweli tukisema tulikusa hapa tarehe mbili ama tulisema tarehe kumi. Mnacheka? Halafu mnaangalia vile tumeandika kama inalingana na maoni yenu. Ninasema mtasoma kwa siku sitini lakini pengine itafupishwa nathani uwe mwezi moja.

Kama ni mwezi moja ama ni miezi miwili, Co-ordinators na wale waalimu wote watatakiwa warudishe hizo nakala hapa, musome hapa tena – round nyingine ya civic education. Halafu ilitakiwa kwamba sisi turudi tena Faza lakini haturudi constituency, tunarudi kwenye mikoa. Kama sasa tutakuja Mombasa kwa watu wa Coast Province. Mkiona tulikosea kabisa, mnatumma mwakilishi wenu, ama waakilishi waje Mombasa waseme nasi. Waseme: kweli muliandika report tarehe ndio hiyo hiyo, lakini yale tulioyasema mumekosea, pengine hiyo itatolewa.

Lakini baada ya haya yote tunaenda kwa mkutano wa taifa, na tulisema wajumbe ama watu watakoohudhuria watakuwa ni watu kama mia sita, kaki yao ni wajumbe wote, all the MPs. Kwa hivyo mjumbe wenu anatakiwa awe kama watchman wenu

kwa huyo mkutano, kusema kama hakutosheka vile tumeandika, ye ye aseme kwa mkutano wa taifa. Tena kila district, itakuwa na waakilishi watatu, mmoja lazima awe ni mama. Kwa hivyo tunaweza kuanza wakati huu kutafuta mama yule ambaye anaweza kuongea. Kwa ajili kwenda kwa hiyo conference ni kama kwenda Bunge. Ni kujadiliana na ndio yule mtu ambaye anaweza kuongea ndio anatakiwa aende. Tusingeme tu mama kwa ajili anapendwa area hii, yule mama ambaye ni sharp kabisa kwa kuongea. Mama mmoja, kati ya hawa watu watatu, mmoja anaweza kuwa councillor. Kama councillor ni mmoja wasizidi hio nambari, na mtu mwingine wa tatu, watu watatu yaani jumla ni hawa wataenda kwa Conference. Mnaweza kupatia maoni hao watatu, kuwaeleza wachunguze kwa makini kama maoni yenu yamewekwa kwa katiba.

Sijui kama Lamu district, is it a new district ama ni ya zamani?

(Answer from the floor: Ni ya zamani)

Kwa ajili kuna kesi kortini sijui kama mnajua? Kuna MP wa Kangema anasema kwamba kuna wilaya zisizo halali, ziliundwa kinyume cha Katiba. Kwa maoni ya huyu mheshimiwa, hawa watu wasihudhurie Conference - - sio wajumbe wao wala waakilishi. Kwa ajili anasema haya yote yalifanywa kinyume cha sheria. Lakini kama district ilikuwa tangu mwanzo, nyinyi hamna shida, bora mtume hao watu watatu - - Yaani MP halafu watu watatu waakilishi wa district.

Halafu tena kuna waakilishi wa vyama vyaya kisiasa ambavyo vilikuwa vimesajiliwa mwezi wa kumi mwaka wa elfu mbili. Sasa vyama ambavyo viko area hii, wajumbe wa hivyo vyama, wataenda tena kama waakilishi wenu. Mnaweza kuitisha maoni tena kwao.

Halafu la mwisho ni kwamba mtakuwa na waakilishi wa civic society: makanisa - dini ya kiislamu, wakristu wa dhehebu tofauti tofauti, vyama vyaya akina mama, NGOs na kadhalika. Kwa hivyo maoni yenu hayataishia hapa munaweza bado kuendeleza mpaka kwa hiyo Conference.

Kama kwa Conference tutakuwa na kutofautiana kwa maswala ya ki-Katiba: Tuseme maneno ya akina mama (vile huyu jamaa alisema) pengine yataingizwa kwa Katiba, lakini akina mama waseme yawekwe ukurasa wa kwanza, na wengine waseme ukurasa wa kumi, lakini wamekubaliana kwamba yawekwe hayo yataamuliwa kwa kupiga kura, yaani simple majority. Lakini maswala ya ki-Katiba, kwa mfano 30% ya wabunge wawe akina mama ama la, au tuwe na serikali ya majimbo ama la. Sasa kama hawatakubaliana kwa Conference kutakuwa sasa na kura ya maoni, kama hizi kura za uchaguzi mkuu. Lakini sasa itakuwa ni maswala matatu manne kwenye makarasi kwa mfano: Je, Kenya iwe na serikali ya majimbo? Na inasema yes or no, muweke X. Kwa hivyo tena wakati huo maoni yenu lazima muyaseme. Hivyo ni kusema uwe tayari kupiga kura baada ya kura ile ya kawaida, ama kabla ya hiyo kwani sijui itakuwa lini.

Kwa hivyo muendelee kuyafwata kwa makini hayo mambo, na musikie vile provinces zingine wanasesma, ndio mujue kama

mapendekezo yenu yatapata support, kwa ajili ni kusikilizana, inaitwa consensus, kama ni simple majority - - watu mia tatu na moja kama ni watu mia sita, na maswala ya ki Katiba - - tuseme two thirds yaani watu mia nne kati ya mia sita. Kwa hivyo mtawezza kutick yale maneno kuhusu ukame, North Eastern hatupingi, hili North Eastern wamesupport, Rift Valley wamesema ni sawa, yaani mnafanya tena campaign kidogo kidogo. Ndio hayo nilitaka kuongeza. Asanteni

**Bwana DO :** Asante sana Daktari Arap Korir. Wazungu wanasesma ‘experience is the best teacher’ kwa hivyo vile mumekuja Faza Island, iangalie vile iko, unapata kuna watu na tunaishi nao. Sitaki kuchukua muda mrefu, nafikiria maoni mengine yenye yalitolewa, hasa kama ya councillor Haji. Yake nafikiria ilikuwa kuhusiana na Hon. Nicholas Biwot. Yale yalikuwa yake na fikiria na ikitoka hapa sifikirii pengine ni kitu tunaweza kuongea.

Nataka kuita Ustadh moja, vile tulianza na dua, atufungie mkutano wa leo na mkienda nyumbani mtaenda salama salimini. Mkikutana na Commissioner, wasalimie, waangalie kama ni wageni wetu, shida zenye wako nazo, tujaribu kuangalia. Mimi mwenyewe ninajua maji yameenda na ninaangalia kama iko. Ustadh Zakaria.

**Ustadh Zakaria :** Nilikuwa na swali la kuuliza --- kulingana na mazungumzo ambayo tumekua nayo.

**Bwana DO :** Nafikiria wakati wenye tutakuwa tumefunga mkutano, tufunge na uwe umeisha.

**Ustadh Zakaria :** Dua la Kisamu kwa lugha ya kiarabu.

Meeting ended at 5.30 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&